# Nipashe

Jumatatu Oktoba 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580054

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wazazi wanavyovutishwa bangi na watoto wao Dar

UKURASA 4




UKURASA 13

# Uvujaji wa mitihani watafuna mabilioni

**NECTA** yafichua gharama zinazopotea kutunga, kuchapisha upya...*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**VYAMA UPINZANI VYAELEZA MAANDALIZI UCHAGUZI MITAA**
VYAMA vya siasa vimeeleza kukamilisha maandalizi ya...

**UKURASA WA 3**

**KATONI 328 POMBE BANDIA ZANASWA**
MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Geita imekamata katoni...

**UKURASA WA 7**

**MLINZI MATATANI KWA TUHUMA KUUA KWA RISASI**
JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia...


## MAGUFULI AFICHUA MAPYA KOROSHO

UKURASA 2



Rais John Magufuli akizungumza baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## CCM walivyochagua wagombea S/ Mitaa



UKURASA 2

MICHEZO **VAR KUTUMIKA SIMBA VS YANGA** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

# JPM afichua mapya wizi fedha wakulima korosho

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), inawashikilia viongozi wa vyama vya ushirika 92 mkoani Mtwara kwa tuhuma za kuwadhulumu wakulima wa korosho Sh. bilioni 1.2.

Amesema fedha hizo ni malipo ya korosho katika msimu wa mwaka 2016 hadi 2017, amewaahidi wakulima hao watalipwa fedha zao.

Aliyasema hayo jana, Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati akiwaapisha viongozi aliowateua mwishoni mwa wiki.

"Juzi nilikuwa Mtwara, Brigedia Jenerali Mbungo (Kaimu Mkuu Takukuru) anafahamu tulikuta malalamiko sana ya baadhi ya watu waliodhulumiwa malipo yao ya korosho kuanzia mwaka 2016 hadi 2017," alisema na kuongeza:

"Na vilikuwa ni vyama vya ushirika 10, baada ya kumwagiza Brigedia Jenerali, akakuta ni vyama vya ushirika 32 ambavyo vilikuwa vinawadhulumu watu. Tulidhani walikuwa wamedhulumu Sh. milioni 80 tukakuta wamezdhulumiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.2."

Rais Magufuli alisema Takukuru imeweza kuwashika viongozi wa Amcos 92 na mpaka juzi walipokuwa wanampatia taarifa (Rais Magufuli) zilikuwa zimerudishwa Sh. milioni 255, na kwamba zilizobakia zinaendelea kurudishwa.

"Mnaweza kuona mtu amelima korosho zake, ameuza, amedhulumiwa na chama cha ushirika tangu mwaka 2016. Anadai amekata tamaa, hawezi kuzipata tena, zaidi ya Sh. bilioni 1.2 zilikuwa katika vyama vya ushirika," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Unaweza kuona ni namna gani dhuluma inatendeka kwa wanyonge, sisi viongozi tunajukumu la kuwatetea wanyonge. Na Brigedia Jenerali amenihakikishia fedha zote watazitema," alisema Rais Magufuli.

**AWAPA MAAGIZO WATEULE**

Aidha, Rais Magufuli aliwapa maagizo wateule hao kwa kuwataka kwenda kusimamia haki, sheria pamoja na kuwatumika wananchi.

"Ni matarajio mtakwenda kutimiza wajibu wenu vizuri sana. Mkakumbuke miiko yenu mliyoifanya hapa, ili kusudi mkayatimize kwa ajili ya wananchi... kazi za watu ni utumwa. Mkawatumikie Watanzania, kila mmoja katika eneo lake, kazi zinachangamoto kubwa, lakini kikubwa mkamtangulize Mungu na kufanya kazi zenu bila ya kumwonea mtu," alisema Rais Magufuli.

Aidha, alimwagiza Mathias Kabunduguru ambaye alimteua kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania kwa kumtaka kwenda kusimamia programu mbalimbali.

"Umefanya mambo mengi utumishi na ulikuwa unatusaidia Tamisemi, ninaamini kule mahakama utaenda kutusaidia vizuri, rekodi yako haina mashaka. Kaendeleze kazi nzuri zinazofanywa na mahakama, kuna programu ya Benki ya Dunia nenda kaiendeleze," alisema Rais Magufuli. Vilevile, alimwagiza Godfrey Mweli ambaye alimteua kuwa Naibu Katibu Mkuu Tamisemi (anayeshugulikia elimu) kwenda kusimamia maslahi ya walimu pamoja na utendaji mzuri katika elimu.

Rais Magufuli alimtaka Mweli kwenda kusimamia kero zote za elimu, za shule, madarasa, walimu, maabara, kero za walimu hasa madai yao, promosheni zao.

Alimweleza kuwa hakuna sababu za walimu kulalamika wala kutokupata huduma zao kwa haraka. Alimtaka kwenda kushirikiana na Waziri wa Tamisemi na makatibu wakuu wa wizara hiyo.

# Uvujaji wa mitihani watafuna mabilioni

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

BARAZA la Mitihani la Taifa (NECTA) limesema kuwa serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa kutokana na uvujaji wa mitihani.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, andiye aliyebainisha ukubwa wa gharama za kutunga mtihani mpya kwa kutolea mfano kwa shule za msingi kuwa Sh. bilioni 100 zimekuwa zikitumika kutunga na kuchapisha mtihani wa shule hizo.

Kufuata hali hiyo, amewataka walimu kuzingatia uadilifu katika usimamizi wa mitihani ili waweze kuinusuru serikali kupata hasara hiyo.

Akizungumza jana jijini hapa katika kikao cha dharura cha Baraza la Taifa la Chama cha Walimu Tanzania (CWT), alisema sheria ya mtihani kuvuja ni lazima ufutwe, hivyo ili kunusuru upotevu wa fedha, na kwamba ni lazima walimu ambao ni maofisa wasimamizi wa mitihani wazingatie maadili ya kazi katika usimamizi wa mitihani.

"Walimu ni watu muhimu sana katika mitihani, hivyo mkiwa waaminifu mtafanya taifa liwe na heshima katika sekta ya elimu hususani katika mitihani inayofanyika," alisema Dk. Msonde. Alisema lengo lao ni kuona Taifa linapata heshima ya kutuvujisha mitihani jambo ambalo linawapa heshima walimu pamoja na taifa kwa ujumla kwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kinaongezeka, lakini kwa akili zao.

Akizungumzia malalamiko ya posho za walimu ambao ni maofisa wasimamizi wa mitihani, Dk. Msonde alisema utungaji wa mitihani na usimamizi hauna posho na kama ipo ni ya siri, na kuwa huwa haitangazwi wala kujulikana katika vyombo vya habari kwa sababu tukio lenyewe ni la siri.

"Mtihani ni siri hata malipo yake kama yapo ni siri na kiwango hakipaswi kujulikana kwa sababu ni tukio maalumu linapaswa kubaki siri," alisema Dk. Msonde.

Akizungumzia suala la uhakika wa vyeti vya walimu, Dk. Msonde alisema kati ya walimu 290 ambao ni wanachama wa CWT waliofanyiwa uhakiki, ni walimu 30 ndio walikutwa na vyeti feki, lakini kati ya hao walimu sita walikata rufani, ambapo mmoja kati yao ndiye alifanikiwa kurejeshwa kutokana na yalifanyika makosa.

"Kazi ya uhakiki ilikuwa ngumu sana kwa sababu wengi waliokuja kukata rufani walikuja na vyeti vingine ambavyo ni tofauti vilivyowasilishwa na waajiri wao," alisema Dk. Msonde.

Aliongeza: "Ukiacha hayo nawapongeza CWT kutokana na heshima ya maadili ya kazi wanayozidi kuionyesha na kuipa heshima sekta ya walimu. Naomba niwapongeze CWT kutokana na mnavyosimamia maadili, safari hii mitihani iko vizuri mmefanya baraza lionekane kuwa na heshima."

Kwa upande wake, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alimshukuru Dk. Msonde kwa ufafanuzi alioutoa kuhusiana na madai ya posho za usimamizi wa mitihani na kuwataka kuwa wavumilivu kwa sababu ni siri.

Hata hivyo, CWT wameiomba serikali kusimamia suala la upandishwaji madaraja ambao inaenda sambamba na upandishwaji mishahara.

Leah alisema walimu wengi wamekuwa wakipandishwa madaraja, lakini mshahara haupandi huku mwalimu mlengwa akiendelea kutumikia nafasi hiyo kwa muda mrefu.

"Tunaomba serikali isimamie hilo, tukipandishwa daraja na mishahara upande," alisema Leah.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Rais Ali Mohamed Shein, akizungumza na kufungua Kikao cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM Zanzibar kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar jana. Kulia kwake ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA: IKULU**

# CCM walivyochaguana uchaguzi serikali mitaa

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa kuwateua wagombea kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), maeneo mengi ukielezwa kutawaliwa na amani na utulivu.

Hata hivyo, katika Kata ya Kiburugwa iliyopo Mbagala Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam, imeelezwa kutokea vurugu, baada majina ya wagombea kutofahamika kwa wajumbe wanaotakiwa kupigakura.

Akizungumza na gazeti hili kwa simu jana mmoja ya wajumbe wa chama hicho, alidai kuwa wajumbe wa chama hicho katika tawi hilo, walifika mapema kwa ajili ya uchaguzi huo, lakini walishangazwa na kitendo cha majina ya wagombea kutokubandikwa hadharani.

"Tulikuwa pale tangu saa 2 asubuhi tukisubiria majina yabandikwe tuwajue wagombea, lakini baada ya muda lilibandikwa jina moja tu, kitu kilichotushangaza na kutukwaza sana kwa kuwa ni kinyume cha utaratibu," alisema.

Kwa mujibu wa mjumbe huyo, kata hiyo ina matawi manne ya chama hicho ya Kingugi A, Kingugi B, Mkololo na Kikwete ambayo yote yalitakiwa kufanyiwa uchaguzi wa ndani ili kupata wagombea wa nafasi mbalimbali.

Diwani wa Viti Maalum katika kata

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Sehemu ya barabara ya Mbagala Kiburugwa wilayani Temeke iliyojengwa hivi karibuni ikiwa imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Katoni 328 pombe bandia zanaswa

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Geita imekamata katoni 328 za pombe bandia aina ya kasi vodka na Wakawaka Gin zilizokuwa zinaandaliwa kusambazwa kinyemela sokoni bila kulipa kodi.

Pombe hiyo inadaiwa kukamatwa na maofisa wa mamlaka hiyo juzi baada ya kuwekwa mtego kwa wafanyabiashara wanaosambaza vinywaji vya aina mbalimbali mkoani hapa.

Meneja wa TRA mkoani Geita, Hamisi Ngoda, akizungumza na gazeti hili, alisema katoni 230 za pombe hizo zilikamatwa na maofisa wa mamlaka hiyo zikiwa kwenye gari moja aina ya Toyota lenye namba za usajili T396 DFC mali ya kampuni ya( KASI PLUS (T) LIMITED) inayotengeneza pombe hizo, na baada ya kukaguliwa lilikutwa likiwa limesheheni katoni 230 za pombe hiyo ambazo zilikuwa tayari kuuzwa kwa wafanyabiashara hao.

Meneja huyo alisema kuwa katoni 97 za pombe hizo zilikamatwa na maofisa wa mamlaka hiyo kwenye maduka ya wafanyabiashara wawili ambao ni wasambazaji wa vinywaji vya pombe za aina mbalimbali wa mkoani Geita, na kuwa a mzigo huo unatakiwa kulipa kodi ya zaidi ya Sh. milioni 7.

Aidha, Ngoda alisema mamlaka hiyo inalishikilia gari la kampuni hiyo na wafanyabiashara wawili ambao hapa msambazaji wa pombe hizo na dereva wa gari hilo, na kuongeza kuwa uchunguzi unaendelea kwenye kiwanda cha kampuni hiyo Kibaha.

Pia aliwaonya wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi ya serikali mkoani humo kuwa mamlaka hiyo imejipanga kuwadhibiti kikamilifu.

# Vipodozi 16 vyaondolewa madukani Dar es Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

MAOFISA wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamefanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya vipodozi na kuondoa aina 16 za vipodozi vilivyopigwa marufuku kwa matumizi ya binadamu.

Vipodozi vilivyoondolewa kwenye soko vinaelezwa kuwa na viambata vyenye sumu hivyo kuhatarisha afya kwa watumiaji.

Maofisa hao walifanya ukaguzi huo mwishoni mwa wiki kwenye maduka mbalimbali yaliyopo Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ukaguzi huo, Mkaguzi Mwandamizi wa Shirika hilo, Mhandisi Donald Manyama, alisema wauzaji wa vipodozi hivyo wameonyesha ushirikiano wa kutosha kwani wamevitoa kwa kadri ambavyo walielekezwa.

Alipoulizwa kama kuingia nchini kwa vipodozi hivyo, kunachangiwa na kutokuwapo udhibiti wa kutosha mipakani, Mhandisi Manyama alisema udhibiti upo wa kutosha, lakini vitu ambavyo vimepigwa marufuku nchini vinaingia kwa njia ambazo siyo halali.

Alisema waingizaji wamekuwa wakitumia njia za panya kuingiza vipodozi hivyo na kwamba vile walivyonikamata wamevichukua kwa ajili ya kwenda kuviharibu.

"Operesheni hiyo siyo kwamba itaishia hapa Dar es Salaam, baada ya kumaliza hapa tutaendelea na ratiba yetu mikoani kuondoa vipodozi hivi," alisema Mhandisi Manyama.

Kuhusu madhara ya vipodozi hivyo vyenye viambata sumu kwa matumizi ya binadamu, alisema vina madhara kwenye ngozi ya binadamu.

"Kwanza vinaichubua ngozi na kuifanya kuwa laini kiasi kwamba mtumiaji akifanyiwa operesheni ushonaji wake unakuwa ni mgumu," alisema na kuongeza;

"Vingine vinasababisha saratani, hivyo tunawashauri hata watumiaji kuacha kutumia vipodozi hivyo. Wengine wanavitumia bila kufahamu wakiona mwenzao amebadilika ngozi wanadhani havina madhara," alisema.

Alisema wataendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waache kutumia vipodozi hivyo na alitoa wito kwa wasambazaji wa vipodozi hivyo kuacha kwani wakikamatwa mitaji yao itapotea na watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini.

Baadhi ya vipodozi vilivyokamatwa kwenye ukaguzi huo na kuondolewa sokoni ni Carolight, Movate, Coco Pulp, Diproson,Viva White, Carotone, Bronz na Eclair.

Vingine ni Citrolight, Tent Clear, Tender White, Clinic Clear, TCD, Baby Face, Light up, Dermotyl na Top Lemon.

Mmoja wa wauzaji wa vipodozi hivyo, Rose Joseph, alishauri udhibiti uimarishwe zaidi mipakani kwani kama vitaendelea kupatikana vitazidi kupata soko.

# Vyama vya upinzani vyaeleza maandalizi uchaguzi mitaa

**Na Enock Charles**

VYAMA vya siasa vimeeleza kukamilisha maandalizi ya wagombea kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu nchi nzima vingine vikieleza changamoto mbalimbali za kikanuni katika maandalizi hayo.

Akiongea kwa njia ya simu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vincent Mashinji, alisema chama hicho kimeshapata wagombea katika uchaguzi huo nchi nzima na sasa kinasubiri siku ya kupewa fomu za serikali.

"Sisi tayari tunao wagombea nchi nzima na tunachosubiri ni siku tu ya kuchukua fomu za serikali kwa wagombea wetu," alisema Mashinji.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema chama hicho kimeshaandaa wagombea wanaotarajiwa kuchukua fomu za serikali na kinachosubiriwa sasa ni siku ya kuchukua fomu hizo.

"Tumejitahidi kila hatua muhimu kuanzia katika zoezi la uandikishaji nadhani umeona tulivyotumia uwezo wetu kuhamasisha na wagombea tumeishawaandaa tunasubiri tu siku ya kutolewa kwa fomu za serikali," alisema Ado. Kuhusu changamoto katika maandalizi ya kuelekea uchaguzi, mwenezi huyo alidai kuwapo kwa changamoto ya kupata mihuri katika ngazi za matawi kutokana na gharama za kutengeneza mihuri hiyo kwa kila tawi.

"Zamani ilikuwa mgombea anaweza kugongewa muhuri katika ngazi ya jimbo ama wilaya, lakini kutokana na kanuni mpya ni lazima kupata muhuri wa ngazi ya tawi, sasa fikiria una matawi zaidi ya 20,000 nchi nzima mara 5,000 au 10,000 ya muhuri," aliongeza Ado.

Kwa upande wa Chama cha Wananchi CUF, Mkurugenzi wake wa Habari na Uenezi, Abdul Kambaya, amesema chama hicho kimeshapata wagombea na sasa wanaendelea na uhamasishaji wa viongozi pamoja na wagombea katika chama hicho ili kuhakikisha chama hicho kinaibuka na ushindi mnono katika uchaguzi huo.

"Tunaendelea na uhamasishaji na sasa nipo mikoani nishamaliza mikoa mitano na bado naendelea lengo ni kuhakikisha tunapa ushindi katika uchaguzi," alisema Kambaya.

Akizungumza na vyombo vya habari wiki iliyopita, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema watu milioni 19.7 sawa na asilimia 86 wamejitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Tamisemi, uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu huku fomu za serikali kwa wagombea zikitarajiwa kutolewa Oktoba 29 hadi Novemba 4.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, pia uteuzi wa wagombea utafanyika Novemba 5 mwaka huu na kampeni kuanza Novemba 17 hadi Novemba 23 kabla ya uchaguzi kufanyika Novemba 24, mwaka huu nchi nzima.


**TANGAZO KWA UMMA**

**MATUMIZI MABAYA YA JINA LA**

**BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA KWA UDANGANYIFU**

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

**Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:**

- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya **barua-pepe: security@afdb.org.**

215468802

# Wazazi wanavyovutishwa bangi na watoto wao

## •Mabegi ya watoto wa chekechea yatumika kubeba 'unga'

**Na Romana Mallya**

MATUMIZI ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana walio katika umri wa kwenda shule ni changamoto kubwa katika familia nyingi jijini Dar es Salaam.

Pia kutokana na jitihada za serikali kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini, baadhi ya wazazi na walezi wamejikuta wakivutishwa moshi wa bangi na watoto wao ambao wamelazimika kuwa wanavuta bangi nyumbani badala ya vijiweni ilivyokuwa zamani.

Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa Kinondoni Shamba jijini Dar es Salaam, Chau Timbuka, aliiambia Nipashe katika mahojiano maalumu kuwa matumizi ya dawa za kulevya ni changamoto kubwa katika mtaa wake huo.

Alisema anasikitika kuona vijana wenye umri mdogo wa kuanzia umri wa miaka 12 wamejiingiza kwenye matumizi ya bangi na aina nyingine za dawa za kulevya.

"Tumefanya mikakati mbalimbali ili kudhibiti wimbi hili la vijana wadogo kutumbukiwa kwenye uvutaji bangi, lakini tumekwama, tunahitaji msaada zaidi ili tuwanusuru vijana wetu.

"Baadhi yao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wanavuta bangi, wanakamatwa, lakini wakifikishwa polisi, wanakaa muda mfupi unawakuta tena mtaani, hii naona ni tofauti na watu wanaokamatwa na Cocaine au Heroine. "Changamoto iliyopo ni kwamba baadhi ya wazazi ni miongoni mwa wanaotumia dawa hizi, wazazi walio wengi ni vijana, wamekulia katika changamoto hii, mwisho wa siku wanashindwa kuwadhibiti watoto wao. Unakuta mtoto wa darasa la tano anavuta bangi na mzazi ameshindwa kupambana naye.

"Imefika hatua mtoto ndiyo mwenye sauti kuliko mzazi. Mzazi hawezi kumkemea mtoto wake wala kumshurutisha au kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola kuhusu tabia ya mtoto wake anayetumia au anauza bangi licha ya shughuli hiyo kufanyika nyumbani kwake, baadhi ya wazazi wanahofu kwa sababu vijana wana makundi hatari. "Imefikia hatua mtoto anamshikia panga mzazi au mlezi wake kisa anamkemea na kumtaka aachane na bangi. Wakati mwingine wamekuwa wakipuliziwa moshi wa bangi, jamii kwa ujumla imeingiwa na uoga na mwisho wa siku ukimuuliza mzazi kuhusu mtoto wake, anakujibu amemwachia Mungu," alisema.

Alibainisha kuwa mtaa wake huo una jumla ya wakazi 10,558, kati yao, vijana ni zaidi ya 3,000 na wengi wao hawajishughulishi na shughuli halali za kuwaingizia kipato.

**BEGI LA CHEKECHEA**

Timbuka alisema kuwa mwaka jana, walifanya msako kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na walibaini baadhi ya vijana wamekuwa na mbinu za kuficha bangi na aina nyingine za dawa za kulevya kwenye mabegi ya wanafunzi wa madarasa ya awali, maarufu chekechea.



RPC wa Kinondoni, Musa Taibu.

"Wakati tunafanya msako, tuliingia kwenye nyumba moja tukakuta watoto wa mwenye nyumba wakiwa wameficha mzigo wa bangi kwenye begi la madaftari ya mdogo wao aliyekuwa akisoma darasa la awali. Walifanya hivyo wakidhani polisi wasingehangaika na kukagua begi la mtoto," alisema.

"Wanavuta bangi nyumbani kwa wazazi wao, wakionywa wanawatishia maisha, mwisho wa siku wazazi wamekuwa waoga kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola, wanaishia kuvuta moshi wa bangi unaotoka vyumbani kwa watoto wao kila siku."

Timbuka alisema yale makundi ambayo yalikuwa yakionekana mtaani yakivuta bangi kwenye vijiwe, kwa sasa yamehamia kwenye baadhi ya nyumba ambazo wazazi wamewapa vyumba watoto wao.

"Mzazi anampa mtoto wake chumba kwa ajili ya kulala, lakini kinachotokea kinageuzwa na kuwa kijiwe cha kuvuta bangi, hii ndiyo changamoto kubwa ambayo tumebaki nayo, tunaomba vyombo husika waje watusaidie," alisema.

"Tumekuwa na operesheni mbalimbali za kukamata watoto ambao hawaendi shule, kila mara tumekuwa tukiifanya, tunapita kwenye nyumba ambazo tunazijua wana watoto wenye umri wa kwenda shule kuhimiza waende shuleni. Huwa tunakamata wazazi, hii imesaidia kidogo."

**WAZAZI WANENA**

Sam Mrope, mmoja wa wazazi katika mtaa huo, aliiambia Nipashe kuwa katika familia yake, anaishi na ndugu zake wawili wanaotumia bangi na mara kwa mara wamekuwa wakikamatwa na polisi na baadaye huachwa huru.

"Imefikia hatua nimechoka kwa sababu unakuta wanavuta hapa, halafu kuna watoto na sisi wazazi, wakati mwingine nikipata hasira huwa ninawaeleza kuwa nitakwenda kuita polisi," alisema.

Mrope anasema vijana wanaipenda bangi kwa sababu bei yake ni rahisi, akidai kuwa kete moja huuzwa kati ya Sh. 400 hadi 500 na inaweza kutumiwa na wavutaji wawili na ikakata hamu yao kwa muda.

"Mara nyingi huwa ninashinda hapa dukani, asilimia kubwa ya wanaofika hapa ni watoto ambao huja kununua sigara kali ambayo ndiyo hutumika kuchanganya na bangi. Kwa siku, si chini wa watoto 10 ambao wanakuja kununua sigara moja hadi tano."

"Ukikaa ndani ya saa moja hapa dukani wanaweza kuja kwa nyakati tofauti watoto wenye umri kuanzia miaka 12, wanataka sigara kali na moja huuzwa Sh. 200.

Mrope alibainisha kuwa ili kupata fedha, watoto hao wamekuwa wajiunga kwenye makundi, baadhi yao wakiokota vyuma chakavu na kuuza na wengine nyakati za usiku wamekuwa wakienda kwenye vigodoro au baa kuiba chupa za bia na kuziuza sehemu nyingine.

"Binafsi nilikuwa na mpwa wangu ambaye akiwa kidato cha kwanza hadi cha pili alikuwa anafanya vizuri, lakini alipofika kidato cha tatu mwishoni, alimpata mvuta bangi maarufu eneo hili ambaye alimlaghai na mwisho wa siku alipata ujauzito na kuacha shule," alisema.

"Kabla ya ujauzito, nilijaribu kuingilia kati ili kuvunja ule uhusiano, lakini bibi mzaa baba wa huyo binti, alinitaka niache nisijepata matatizo kwa kupambana na mvuta bangi."

Delifina Makwinya, mzazi pia katika mtaa huo, anasema kutokana na kasi ya ongezeko la vijana wanaovuta bangi kwenye maeneo hayo, amelazimika kumtoa mtoto wake kwenye shule ya kutwa na kumpeleka shule ya bweni.

Makwinya ambaye ni mjumbe wa eneo hilo la Kinondoni Shamba, alisema katika eneo lake hilo analolisimamia hali ni mbaya na baadhi ya vijana wanaotumia bangi wamejiingiza kwenye uhusiano wa jinsi moja (ushoga).

"Watoto wanajiingiza huko kwa sababu ya tamaa ya maisha na wengine wanaingia kwa sababu ya makundi ambayo yameshaharibikiwa mtaani, unakuta mtoto alikuwa anasoma na alikuwa akifanya vizuri tu, lakini baadaye anatumbukia kwenye uvutaji bangi," alisema.

"Nimekuwa na utaratibu kila mwezi mara moja au mbili nazitembelea familia za watoto walioathirika kutokana na matumizi ya dawa za kulevya ili kusaidia kutoa elimu."

**ULINZI SHIRIKISHI**

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Hananasif, Kata ya Hananasif jijini, Seleman Lada, aliiambia Nipashe kuwa katika mtaa wake kwa sasa hali ni shwari baada ya kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi kukabiliana na vitendo hivyo na uhalifu mwingine uliokuwa umeshamiri.

"Vikundi hivi vimekuwa vikikabiliana na wizi, pombe haramu na dawa za kulevya, hupita nyumba kwa nyumba kuangalia. Waliokuwa wakitumia dawa za kulevya katika mtaa wangu, tuliwapata, watano ambao wanaendelea na matibabu ya Methadone katika Hospitali ya Mwananyamala," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kawawa, Kata ya Hananasif, Elizabeth Masao, alisema mtaa wake ulikuwa ukisifika kwa vijana maarufu wakata mapanga, maarufu 'Panya Road' wenye umri kati ya miaka 12 na 15 ambao walikuwa wakijihusisha na vitendo vya kutumia dawa za kulevya.

"Mbinu ambayo tumeitumia kuyamaliza makundi haya ambayo yalikuwa ni hatari na tishio, ni kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi ambavyo viliwakamata mmoja baada ya mwingine na kama kuna wanaoendelea na matumizi ya dawa za kulevya, watakuwa wanafanya hivyo kwa vificho vya hali ya juu," alisema.

**MAENEO KOROFI**

Ambani Famili, mratibu wa mafunzo wa asasi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utoaji elimu kuhusu athari zitokanazo na dawa za kulevya, alizungumza na Nipashe na kuyataja maeneo mengine ambayo bado yana changamoto za dawa za kulevya kuwa ni Msasani, Tegeta, Bunju, Kigamboni na Magomeni Kagera.

"Maeneo hayo bado tunaendelea kutoa elimu kwa waathirika ili waanze kutumia Methadone," Famili alisema.

**KAULI YA POLISI**

Nipashe pia ilimtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mussa Taibu, kuzungumzia changamoto hiyo na alikiri mkoa wake kuwa na changamoto hiyo ya matumizi ya dawa za kulevya.

"Dawa za kulevya Kinondoni siyo suala la leo, hili ni tatizo la muda mrefu, na siyo kwamba halifanyiwi kazi, tunafanya kazi sana kwa ushirikiano wa Jeshi la Polisi, wananchi, serikali za mitaa na polisi jamii wa kila kata ambao wamepewa jukumu la kuelimisha wananchi kuacha dawa za kulevya," alisema.

Kamanda Taibu alisema vijana wadogo wamejiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya aina za bangi, Heroine na Cocaine.

"Watoto wenye umri wa kuanzia umri wa miaka 15 na kuendelea wameathirika kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, hawa wapo kwenye rika ya kubalehe, hivyo ni rahisi kwao kuigaiga vitu. Ipo sheria ya namna ya kuwakamata, kukabiliana nao na kuwasaidia," alisema.

Kamanda Taibu alieleza kuwa wamebaini watoto kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kunasababishwa na wazazi au walezi wenyewe ambao wanakwepa jukumu la kuwalea kwa kuzingatia maadili.

"Wazazi kutojali, kutowasimamia watoto wao ni tatizo kubwa sana kwenye familia. Tatizo lingine, wazazi wa sasa wanashindwa kuwashirikisha watoto kwenye shughuli ndogondogo nyumbani baada ya kutoka shule ili kutoruhusu kuzurura mitaani."

"Hakuna usimamizi wa namna mtoto anakwendaje shule na anarudije nyumbani kwa maana kwamba usalama wake njiani."

"Tabia za watoto wenye rika fulani kuiga wengine waliowazidi umri zinasababisha wanaiga tabia zisizo nzuri likiwamo hili la utumiaji wa dawa za kulevya.

"Wazazi wangekuwa na ukaribu na watoto na kuwasimamia na kuwaelekeza, ingekuwa rahisi kujua mtoto yupo wapi, anafanya nini na yupo na nani."

Kamanda Taibu alisema changamoto nyingine ni wazazi wa sasa kutowajengea watoto wao hofu ya Mungu kwa kupelekwa kanisani na msikitini wakasome elimu ya dini.

**INAENDELEA UK. 8**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
ISO 9001: 2015
IDARA YA KODI ZA NDANI

# TAARIFA KWA UMMA

## WAJIBU WA KUTOA NA KUDAI RISITI/ANKARA ZA MASHINE ZA KIELEKITRONIKI (EFD).

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inapenda kuwataarifu Wafanyabiashara wote na umma kwa ujumla kwamba, kulingana na kifungu namba 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015, kinawataka watoa Huduma au wafanyabiashara wanaostahili kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) kutoa risiti za kielektroniki kwa mauzo yote ya bidhaa au huduma yanayofanywa. Utoaji huu wa risiti za EFD ulianzishwa ili kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Walipakodi, kurahisisha ukadiriaji wa kodi na kuongeza ulipaji kodi kwa hiari na hivyo kuongeza pato la Taifa.

Uchunguzi uliofanywa na TRA umebaini kwamba, baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kutotoa risiti kwa makusudi na wengine kutoa risiti zenye viwango vya chini visivyoendana na gharama ya bidhaa au huduma iliyouzwa. Kitendo cha kutotoa risiti kupitia mashine za Kielekitroniki (EFD) ni hujuma juu ya juhudi za Serikali kukusanya mapato yanayolenga kuleta maendeleo kwa watanzania wote.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuwakumbusha Wafanyabiashara kuwa, kwa mujibu wa kifungu tajwa hapo juu, muuzaji wa bidhaa au mtoa huduma anawajibika kutoa risiti/ankara sahihi kupitia mashine ya kielektroniki (EFD).

TRA, inautangazia umma kwamba, itaendesha msako kwa biashara zote nchi nzima ili kukagua matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na kujiridhisha utekelezaji wa sheria husika. Mfanyabiashara yeyote ambaye atabainika kutotumia vyema mashine hizi katika biashara yake au kukaidi kutimiza wajibu huu wa kisheria atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 3,000,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 4,500,000 /- au kifungo cha miaka 3 jela** au vyote kwa pamoja, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kifungu cha 86.

Pia wanunuzi wote wanatakiwa kudai risiti pindi wafanyapo manunuzi ikiwa ni haki ya msingi kisheria kwa kila manunuzi. kwani kutokufanya hivyo ni kosa linaloweza kupelekea kupata adhabu kali ikiwa ni kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 30,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 1,500,000/-** kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015.

**Taarifa za msingi ambazo risiti/ankara inahitaji kuwa nazo ni pamoja na zifuatazo;**

1. **Jina la Mnunuzi.**
2. **Namba ya usajili ya mnunuzi (TIN)**
3. **Namba ya Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mnunuzi (VRN kwa waliosajiliwa VAT).**
4. **Jina la bidhaa/huduma iliyouzwa au kutolewa.**
5. **Thamani halisi ya bidhaa/huduma iliyouzwa**

Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na kituo cha huduma na elimu kwa mlipakodi kwa kupiga simu za bure: **0800780078 / 0800750075 au Barua pepe Huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Abdul Y. Mapembe**
**KAIMU KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

215466002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi kuelekea fainali CHAN yaanze

**KWANZA** kabisa gazeti hili linapenda kuipongeza Timu ya Taifa (Taifa Stars), benchi la ufundi na viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kufanikiwa kupata tiketi ya kushiriki katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Ilikuwa ni Ijumaa ya Oktoba 18, mwaka huu, kwa wachezaji wa Taifa Stars kuweka rekodi nyingine kwa nchi baada ya kufanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo za CHAN.

Hii ni mara ya pili kwa Taifa Stars kufuzu kushiriki fainali hizo. Mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2008, fainali zilichezwa mjini Abdijan, Ivory Coast na kikosi hicho kilikuwa chini ya Mbrazil Marcio Maximo.

Taifa Stars ambayo sasa iko chini ya Mrundi Etienne Ndayiragije, imefuzu kushiriki fainali hizo baada ya miaka 10, tangu iliposhiriki kwa mara ya kwanza.

Ukionekana kuwa mwaka wa neema kwa Watanzania, mwaka huu pia, Taifa Stars, ilifanikiwa kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), ikiwa imekaa nje ya michuano hiyo kwa miaka 39.

Hiyo ilikuwa ni historia, sasa ni wakati wa kuanza maandalizi kuelekea fainali hizo ambazo zitachezwa Februari, katika miji ambayo itajulikana hapo baadaye.

Februari sio mbali, huu ndio wakati sahihi kwa TFF kuanza kuiandaa timu hiyo ili iweze kwenda katika fainali hizo ikiwa imara.

Si vema Watanzania tukashuhudia timu yetu inapoteza mechi zote za hatua ya makundi, hali ya kuwa muda wa kujiimarisha na kujiweka sawa upo.

Licha ya kukabiliwa na ratiba ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, si jambo baya kama idara ya ufundi itaamua kuangalia nchi nyingine zinavyojipanga, kwa maana ya kuona kikosi cha Taifa Stars kinapata muda wa kukutana na kujifua na vile vile mechi za ligi zikiendelea bila kuwapo kwa malalamiko.

Inawezekana jiografia ya Tanzania inakuwa ni kikwazo, lakini hakuna jambo linaloshindikana kama serikali, ambao ndio wadau wakuu, taasisi na kampuni mbalimbali kukajitokeza kuidhamini timu hiyo kwa lengo la kuhakikisha inakuwa imara na inakwenda kuonyesha ushindani huko Cameroon.

Nipashe tunaamini kuwa mchezo wa soka hauhitaji miujiza, timu inayojiandaa vema ndiyo inayojiweka kwenye nafasi ya kufanya vizuri katika fainali hizo na si kutegemea miujuza.

Siku zote tunakumbushwa kuwa mambo mazuri hutokana na maandalizi sahihi, kuwekeza kuanzia kwenye maandalizi, ndio jambo sahihi na kamwe tuache kusubiri mafanikio au kutoa ahadi za zawadi kwa mchezaji atakayefunga bao, au timu itakapopata matokeo chanya.


Kuwekeza katika maandalizi, kutawafanya wachezaji watakaokwenda katika fainali za CHAN kuwa na viwango bora, na hiyo itaonekana kwenye michezo ya Ligi Kuu Bara ambayo ndiyo inatoa idadi kubwa ya nyota watakaokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo.

Endapo Taifa Stars, itafanya vizuri katika fainali hizo, ina maana wachezaji wengi wa Tanzania watapata timu za nje na watakaporejea, wataisaidia timu hiyo kufanya vema.

Lakini, walengwa ambao ni wachezaji na wanafaidika moja kwa moja, wanatakiwa kujipangia programu zao binafsi ili kuendelea kukuza vipaji vyao.

Kama Algeria na Senegal, ziliweza kufanya vizuri katika fainali zilizopita za Afcon, basi na Tanzania inaweza kufika katika mafanikio hayo, endapo tu, wadau wote watakubali kuwekeza katika mchezo huo, kuanzia ngazi ya watoto na vijana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga isake magoli kuivuruga Pyramids

Na Adam Fungamwango

**YANGA** itacheza mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids kutoka Misri kwenye mechi ya mkondo wa kwanza, hatua ya mtoano, kabla ya timu hizo kurudiana baada ya wiki moja.

Mechi hiyo inatarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza ambako viongozi wa Yanga wameamua waipeleke kwa sababu mbalimbali walizoainisha.

Ni mechi ambayo timu yoyote ikifanikiwa kupata matokeo mazuri kwenye mechi zote mbili za nyumbani na ugenini, basi itatinga moja kwa moja kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga iliingia hatua hii baada ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Zesco ya Zambia, huku Pyramids ikiwa kwenye michuano hii tangu mwanzo.

Ni ukweli usiopingika kuwa ni mechi ngumu kwa wawakilishi hao wa Tanzania, kwani rekodi inaonyesha kwamba timu za Afrika Kaskazini maarufu kama timu za Waarabu huwa zinazisumbua sana timu za Tanzania, lakini Yanga yenyewe imekuwa haina bahati ikikutana na timu za Waarabu kwenye michuano hii mikubwa barani Afrika.

Katika mechi hii ili Yanga ifanye vema, kwanza kabisa ni lazima benchi la ufundi lifanye kazi yake sawasawa na lisiwaaminishe wachezaji kuwa kwa sababu mechi imehamishiwa Mwanza, basi itashinda kirahisi.

Ni lazima machozi, jasho na damu vimwagike kwa pamoja ili kupata ushindi kwenye mechi hiyo, kwa nia moja tu ya kuhakikisha inajiweka vema kwenye mechi ya marudiano ambayo itakuwa ngumu zaidi kuliko hata ya Kirumba.

Wachezaji wa Yanga wacheze soka la kushambulia zaidi kusaka magoli na si kudhani kuwa huwa hawawezi kushinda nyumbani, badala yake hushinda ugenini. Siyo kila siku Ijumaa. Tumeona ilivyotokea nchini Zambia. Na ni ngumu zaidi kushinda nchini Misri, tena kwa idadi kubwa ya magoli.

> **Ni lazima machozi, jasho na damu vimwagike kwa pamoja ili kupata ushindi kwenye mechi hiyo, kwa nia moja tu ya kuhakikisha inajiweka vema kwenye mechi ya marudiano ambayo itakuwa ngumu zaidi kuliko hata ya Kirumba.**

Kwa maana hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, awatengeneze vijana wake wacheze soka la kushambulia muda wote kwa ajili ya kusaka idadi kubwa ya magoli.

Nimeona baadhi ya mechi za Yanga, pamoja na kwamba wana matatizo kwenye nafasi ya ushambuliaji, lakini hata mfumo wenyewe wanaocheza huwa ni wa kujilinda, iwe kwenye Ligi ya Mabingwa au kwenye Ligi Kuu.

Kwenye mechi dhidi ya Coastal Union, Yanga baada ya kupata bao moja, ilionekana kujilinda zaidi kuliko kushambulia, kitu ambacho si cha kawaida sana kwa timu kubwa kama hiyo kujilinda dhidi ya timu ndogo, badala ya kusaka bao la pili.

Mfumo wa kujilinda ndiyo uliioponza timu hiyo kwenye mechi dhidi ya Zesco, kwenye mechi zote mbili ya Dar es Salaam na ugenini. Wakati ikilinda ushindi wa bao moja, ilijikuta ikisawazishiwa bao dakika za majeruhi nyumbani na wakati ikijilinda ikidhani itakwenda kwenye mikwaju ya penalti, ilijikuta ikichapwa bao la pili ugenini.

Bao 1-0 pekee kwenye mechi dhidi ya Pyramids halitoshi, badala yake Yanga inatakiwa ifunge magoli kuanzia mawili na kuendelea, huku isiruhusu wavu wake kuguswa.

Hapo inaweza kujiweka kwenye mazingira ya kuwapa presha wapinzani wao kwenye mechi ya marudiano, vinginevyo hali inaweza kuwa mbaya.

Tunawatakia kila la kheri Yanga, wawakilishi pekee wa Tanzania, waliobakia kwenye michuano hiyo ya kimataifa inayofanyika kila mwaka.

## HABARI KITAIFA



Mwanafunzi wa darasa la sita wa Shule ya Msingi Benjamin Mkapa, Brayson Joseph (13) akiongoza mdahalo uliohusisha vilabu vya wanafunzi wa shule nne za Kata ya Mabogini, Moshi Vijijini kupaza sauti ili kutokomeza ukatili. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Maofisa elimu wawekwa katika wakati mgumu

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tamisemi, George Waitara, amewaweka katika wakati mgumu maofisa elimu msingi na sekondari Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, baada ya kumdanganya kuhusu ukubwa wa eneo la shule ambalo wananchi wamejitolea ili kujenga shule za sekondari na msingi.

Maofisa hao ambao dawa ni Aluko Lukolela (Ofisa Elimu Msingi) na Annastazia Manumbu (Ofisa Elimu Sekondari) ambao wanadaiwa kumdanganya Naibu Waziri huyo aliyefika wilayani Kahama kwa ajili ya kusikiliza na kuutatua mgogoro uliokuwa ukifukuta kwa miaka mitano.

Hali hiyo ilitokana na kutoa taarifa za uongo juu ya maeneo yanayomilikiwa na Shule ya Msingi Majengo huku kila mmoja akitoa takwimu zake, hivyo kutofautiana.

Akiwasilisha taarifa hizo Lukolela alisema eneo linalomilikiwa na Shule ya Msingi Majengo lina ukubwa wa ekari sita, huku Manumbu akimwambia Waitara kuwa ukubwa wa eneo hilo ni ekari 3.5 na wakati huo huo Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Thobias Patrick, aliamua kumweleza ukweli na kitaalamu zaidi Naibu Waziri baada ya kuona mkanganyiko huo na kubainisha kuwa eneo hilo lina ukubwa wa ekari 15. Kufuatia hali hiyo Diwani wa Kata ya Majengo Bernad Mahongo aliangua kilio mbele ya Naibu Waziri akihofia kukwamishwa kwa maendeleo katika kata yake, jambo lililomfanya Waitara kuamua kutembelea eneo hilo na kutoa maelekezo kwa wataalamu wa halmashauri akiwataka kutoa ufafanuzi katika lugha rahisi ili wananchi waweze kuelewa kwa haraka.

"Baada ya kusikiliza malalamiko ya wananchi juu ya kucheleweshwa ujenzi wa sekondari na zahanati katika kata yao nimeona nitoke nikajiridhishe kuhusu utata huo na sasa nimejiridhisha baada ya kutembelea maeneo yote sasa," alisema na kuongeza:

"Naagiza wataalamu wapime eneo kitaalamu ili kubainisha eneo litakalojengwa sekondari, na kuhusu kupata takwimu sahihi zilizotolewa na maofisa hawa ziweze kubainika na ninatarajia baada ya kubaini ukweli atakayekuwa ametoa taarifa za uongo... serikali haitasita kumchukulia hatua stahiki za kinidhamu."

# Mlinzi matatani kwa tuhuma kuua kwa risasi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Ismail Hassan (20), mlinzi wa kampuni ya Sengenti Security Services l.t.d kwa kosa la kumfyatulia risasi ya makalioni kijana mmoja aliyekuwa amevalia kitambulisha chenye jina la Mishael Masatu (29) na kumsababishia kifo.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kubainisha kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 16, alifajiri kwenye yadi ya magari katika kisima cha mafuta cha PetroAfrica Nyasubi.

Alisema Isumail Hassan alimfyatulia risasi moja ya matakoni kijana huyo mwenye kitambulisho cha Mishael Masatu, mkazi wa Kata ya Nyihogo Mtaa wa Sazia kutoka kwenye bunduki aina ya shortgun mali ya kampuni ya Serengeti Services LTD.

Aidha, Abwao alisema chanzo cha tukio hilo ni Masatu kuingia kwenye yadi ya magari katika kisima cha mafuta cha Petro Africa bila kuwa na kibali cha kumruhusu kuingia na kudhaniwa ni mwizi.

Pia alisema baada ya kufyatuliwa risasi hiyo, Masatu alianza kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama na baadaye alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu.

Abwao alisema kuwa mlinzi wa kampuni hiyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kituo kikuu cha Kahama, na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

# Waziri Mkuu kumwakilisha JPM Urusi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, aliondoka nchini jana kwenda Urusi kuhudhuria mkutano baina ya Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa ya Afrika na Urusi utakaofanyika jijini Sochi, Urusi, Oktoba 23 - 24, 2019.

Waziri Mkuu anahudhuria mkutano huo kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, John Magufuli.

Mkutano huo utakaoendeshwa chini ya uenyekiti wa pamoja wa Rais wa Shirikisho la Urusi, Vladimir Putin, na Rais wa Misri, Abdel Fattah el-Sisi, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), unalenga kurejesha na kuimarisha uhusiano baina ya mataifa ya Afrika na Urusi ambao uliyumba baada ya kusambaratika kwa "Union of Soviet Socialist Republic" (USSR) mwaka 1991.

Mkutano huo wa Wakuu wa Nchi na Serikali utafanyika katika sehemu mbili, ambazo ni Kongamano la Biashara (Russia Business Forum) linalotarajiwa kufanyika Oktoba 23, na Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi za Urusi na Afrika uliopangwa kufanyika Oktoba 24, 2019.

Waziri Mkuu atashiriki kwenye mikutano yote miwili.





Mwandishi wa Habari Mwandamizi, Atilio Tagalile, akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari wa vyombo vya habari vya IPP kuhusu namna ya kuripoti uchaguzi, yaliyofanyika Mikocheni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kuwajumuisha waandishi kutoka kampuni ya The Guardian Ltd, ITV/Radio One, EATV, Capital Radio na East Africa Radio. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# CCM walivyochaguana uchaguzi serikali mitaa

**INATOKA UK. 2**

hiyo aliyejitambulisha kwa jina la Mama Shija, alipoulizwa kuhusiana na uchaguzi huo, alitaka atafutwe msemaji wa chama wa ngazi ya wilaya ili kuzungumzia suala hilo.

Nipashe lilimtafuta Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Zakaria Mwansasu, ambaye alisema uchaguzi ulikuwa na hamasa kubwa na idadi kubwa ya wanachama walijitokeza kupiga kura katika mkoa wa Dar es Salaam.

Alipoulizwa kuhusu changamoto zilizojitokeza katika baadhi ya maeneo, Mwansasu alisema CCM ina utaratibu wa kufikisha malalamiko kwa wanachama wake.

"Chama kina kanuni, katiba, kama yupo mwanachama ambaye analalamika hakutendewa haki, anapaswa kufuata utaratibu wa kuwasilisha malalamiko yake," alisema Mwansasu.

Alisema mwanachama anapaswa kuandika barua ya malalamiko yake na kuiwasilisha ngazi husika na kuongeza kuwa pia kuna vikao vipo vya kutatua changamoto au kero zilizojitokeza.

**DODOMA**

CCM Mkoa wa Dodoma imewaonya viongozi wake kutojihusisha na kupanga safu kwa ajili ya chaguzi zijazo kwenye mchakato wa kura za maoni kwa viongozi wa vitongoji, vijiji na mtaa.

Akizungumza jana kuhusu mwenendo wa kura za maoni za kuchagua wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa, Mwenyekiti wa CCM mkoani humo, Godwin Mkanwa, aliwataka wagombea, wanachama na viongozi kuzingatia makatazo yote kipindi hiki cha uchaguzi wa serikali za mitaa ili kutoleta makundi ndani ya CCM.

"Wanachama na viongozi wahakikishe kila mgombea anazingatia kanuni za uchaguzi ambazo zina makatazo ambapo ni pamoja na kutotumia rushwa kwenye uchaguzi, kutumia udini au ukabila, kutumia nafasi yako kiongozi kuwalazimisha wanachama wanaopiga kura za maoni kumchagua mgombea kwa matakwa yako," alisema.

Aliwataka viongozi wasijihusishe na kupanga safu kwa ajili ya chaguzi zijazo kwa kuwa chama kinataka wapatikane viongozi walio bora.

"Wawasikilize vizuri wagombea wanapojieleza na wawapime ili kupata viongozi bora, nawaasa waepuke makundi yasiyo na sababu ambayo baadaye yatatugawa kwenye uchaguzi wa mwisho wa serikali," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kwa mujibu wa kanuni na taratibu za CCM zipo hatua zinazochukuliwa kwa mwanachama na kiongozi atakayebainika kukiuka makatazo ikiwamo viongozi kupoteza nafasi zao.

Kuhusu mchakato wa kura za maoni, Mkanwa alisema ulianza Oktoba 19-20, mwaka huu na utaendelea hadi leo kama kukiwapo na mapingamizi mbalimbali kuhusu wagombea watakaokuwa wameteuliwa.

"Hakuna changamoto yoyote hadi sasa, lakini kama unavyojua ushindani lazima na haukosekani kuna mahali mwingine analalamika jina halikurejeshwa tulikuwa 12 mimi nimeondolewa ni mambo ya kawaida hayo, kwa ujumla zoezi linaendelea vizuri," alisema.

Alifafanua kuwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi kila ngazi wagombea wataomba kwa idadi ya watakaojitokeza, lakini vikao vitachuja na kurejesha majina matatu kwa ajili ya kupigiwa kura za maoni kwa ngazi ya matawi, mashina kwenye kitongoji au kijiji, watatoa mapendekezo yao kumchagua mwenyekiti.

"Kamati za siasa za kila ngazi ndio zimefanya kazi ya kuchuja wagombea ambapo ngazi kitongoji inafanywa na kazi ya kata, ngazi ya kijiji au mtaa kamati za siasa za wilaya ndio zinafanya kazi hiyo baada ya hapo majina matatu yatakayopigiwa kura za maoni majina yale yale yatakuja na kura zake na mapendekezo yake kwa kila ngazi," alisema.

Alieleza baada ya kura hizo ngazi ya Halmashauri Kuu ya kata itatoa mapendekezo kwa mgombea mmoja wa kitongoji kulingana na kura zilizopigwa huku ngazi ya Halmashauri Kuu ya wilaya itatoa mapendekezo kwa mgombea mmoja wa kijiji au mtaa kati ya watatu ateuliwe kulingana na kura za maoni zitakazopigwa.

Kadhalika, mwenyekiti huyo alisema CCM Dodoma imejipanga vyema kuhakikisha inabaki na hadhi yake ya kwamba ni ngome ya chama hicho.

"Uchaguzi wa mwaka 2014 wa serikali za mitaa tulikuwa kidedea na tulishinda kwa takriban asilimia 92, sisi ni ngome ya CCM hatuna shaka na ushindi utakuwa zaidi ya ule kwa kuwa mambo mengi yamefanyika na utekelezaji wa ilani umefanyika vizuri," alisema.

**MBEYA**

Upigaji kura za maoni ndani ya CCM Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa umekamilika kwa asilimia 75.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa Chama hicho Mkoa wa Mbeya, Solomon Itunda, alipokuwa anazungumza na Nipashe ambapo alisema zoezi hilo limefanyika kwa muda wa siku mbili mfululizo.

Alisema mpaka jana jioni makatibu wa chama ngazi ya Wilaya walikuwa wanawasilisha matokeo katika ofisi yake kutoka katika maeneo yao, huku akisema kuwa zoezi hilo lilikabiliwa na baadhi ya changamoto ambazo hata hivyo, hakuzitaja.

"Kwa sasa asilimia 25 iliyobakia ni kupokea matokeo kutoka kwa makatibu wa wilaya ambao ndio wakurugenzi wa uchaguzi kwenye maeneo hayo," alisema Itunda.

Alisisitiza kuwa zoezi hilo lilifanyika kwa haki na uwazi kama katiba na kanuni za chama hicho zinavyotaka.

**KILIMANJARO**

Upigaji wa kura za maoni katika wilaya sita za mkoa wa Kilimanjaro, kwa mara ya kwanza wanachama wake hawajajitokeza kupinga matokeo.

Katibu wa CCM mkoani Kilimanjaro, Jonathan Mabhiya, alisema hadi kufikia jana jioni katika wilaya nne za Moshi, Hai, Siha na Rombo walikiwa hawajapokea taarifa ya kupingwa matokeo.

"Wana chama waliojitokeza ni wengi kwa mara ya kwanza katika mkoa wetu, mpaka sasa hatujapata taarifa za waliokataa kusaini matokeo kutokana na labda kuibuka mizengwe. Wote wamesaini fomu za kukubali matokeo," alisema Mabihya.

**ARUSHA**

WANANCHI wa Mtaa wa Murieti Kata ya Murieti wilayani Arusha, jana wamejitokeza kwa wingi kuchagua wagpmbea.

Diwani wa Kata ya Murieti, Fransis Mbise, alisema uchaguzi huo umekwenda kwa amani, na walikuwa wanaendelea na kuhesabu kura.

"Zoezi lilianza asubuhi, lakini maeneo mengi kutokana na leo (jana) walijitokeza saa tano hadi saa sita kwa wingi na zoezi limeenda kwa amani," alisema.

Alisisitiza anaendelea kufuatilia kuona zoezi hilo linaisha kwa usalama.

**Imeandikwa na Enock Charles na Gwamaka Alipipi, Dar, Augusta Njoji, DODOMA, Godfrey Mushi, Moshi, Nerbet Msoka, Mbeya na Cynthia Mwilolezi, Arusha.**

# Wazazi wanavyovutishwa bangi na watoto wao

**INATOKA UK. 4**

"Familia zenyewe ni matatizo, unaikuta haina tabia njema kabisa, unategemea mtoto atakuwa na tabia nzuri? Hili ni tatizo kubwa," alisema. Kutokana na vijana wadogo kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya, Kamanda Taibu alisema maeneo mengi ya Kinondoni yanakabiliwa na uhalifu wa uporaji wa mali mbalimbali na kuvunja nyumba na kuiba.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko dhidi ya Jeshi la Polisi kutochukua hatua stahiki dhidi ya wanaokamatwa kutokana na kujihusisha na matumizi ya bangi, Kamanda Taibu alisema hakuna mahali ambako sheria imelegea na wamekuwa wajitekeleza vizuri wajibu wao.

"Suala ni kwamba wale wanaosimamia katika kutoa uamuzi, nikimaanisha mahakimu, wasilegeze kamba, kama mtu anatakiwa kufungwa kifungo cha maisha kitekelezwe, kama mtu anafungwa miaka 30 asipate huruma, sheria inayohusu dawa za kulevya ni kali," alisema.

"Sheria ya Dawa za Kulevya haina urafiki kwa mtu aliyekutwa na bangi au dawa za kulevya za aina nyingine ila itategemea amekutwa na ujazo wa kiasi gani.

"Zipo gramu zenye dhamana kisheria na zisizo na dhamana, ukikutwa na kidogo sana ni rahisi kupata dhamana, ukikutwa na kiwango kikubwa ambacho sheria imekataa, kuna gramu zimewekwa, nafikiri ni zaidi ya gramu 28 ukikutwa na kiasi hicho kesi yako haina dhamana. "Bangi zinaletwa kutoka mikoani, mfano Arusha, Tanga na Iringa ambako ndiko inalimwa, watu wengi wanasafirisha kuleta Dar es Salaam." Akizungumzia tukio la Kinondoni Shamba ambalo begi la mwanafunzi wa darasa la pili kutumika kuhifadhi bangi, Kamanda Taibu, alisema wahalifu hao walitumia mbinu hiyo kujihami wakiamini kuwa takwimu zilizopo hakuna watoto wenye umri huo walioathirika na dawa hizo.

"Kuikuta bangi kwenye begi la mwanafunzi wa darasa la kwanza au la pili siyo kitu cha ajabu kwa sababu wanaamini wakificha huko ni sehemu salama."

"Sisi tunapoingia kwenye nyumba kufanya upekuzi, haijalishi ni begi la mtoto wa darasa la kwanza au la mtoto aliyezaliwa jana, tunapekuwa kila kona, lengo ni kwamba tuwe na taarifa kamili nyumba fulani kuna dawa za kulevya," alisema.

**TAKWIMU ZA MATUMIZI**

Takwimu za matumizi ya dawa za kulevya nchini ambazo Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, aliipatia Nipashe, inaonyesha Cocaine zilizokamatwa kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu ni kilo 10 na watuhumiwa 17 (wote wanaume) walikamatwa. Pia takwimu hizo pia zinabainisha kuwa katika dawa za kulevya aina ya Heroine kilo 24.1 zilizokamatwa katika kipindi hicho, watuhumiwa wanaume 358 walikamatwa wakihusishwa nazo wakati wanawake walikuwa 16.

Kwa upande wa dawa za kulevya za shambani (bangi na mirungi), takwimu za Jeshi la Polisi inaonyesha kilo 13,237.7 zilikamatwa zikiwahusisha watuhumiwa wanaume 4,754 na wanawake ni 308. Takwimu za jeshi hilo zinaonesha kuwa katika kipindi hicho cha nusu mwaka, mirungi iliyokamatwa ilikuwa ni kilo 3,846.7, watuhumiwa wanaume waliokamatwa wakihusishwa nayo wakiwa ni 533 na wanawake 122.

Misime alisema kesi kuhusiana na ukamataji huo zilishafunguliwa mahakamani na watuhumiwa 290 wameshahukumiwa adhabu mbalimbali ikiwamo kifungo gerezani.

Alisema Jeshi la Polisi kama mtekelezaji wa sheria mbalimbali kwa kutambua madhara ya dawa za kulevya, limeungana na jamii ya kimataifa kupambana na wahalifu wanaojihusisha na dawa za kulevya.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kulia), akimkabidhi tuzo ya ushindi wa jumla kwa sekta ya uwekezaji katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Uendelezaji Biashara wa TBL Group, Bruno Zembrano, wakati wa hafla ya kukabidhi tuzo kwa wanachama wa soko hilo, iliyofanyika katika hoteli ya Hyatt jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mkama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa aibana mikoa agizo uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka mikoa ambayo bado haijatekeleza agizo lake la kuandaa makongamano ya uwekezaji ihakikishe inafanya hivyo mara moja.

Ametoa agizo hilo leo mchana wakati akifungua Kongamano la Uwekezaji kwa mkoa wa Pwani katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo. "Nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wa mkoa wa Pwani kwa kutekeleza agizo nililolitoa Juni 18, 2018, wakati wa kongamano la tatu la uwezeshaji wananchi kiuchumi la kuhakikisha mikoa yote inaandaa kongamano la uwekezaji na inakuwa na mwongozo wa uwekezaji wa mkoa. Mikoa ambayo haijatekeleza agizo hilo, ifanye hivyo mara moja," amesema. Alisema mkoa huo umeweza kubaini fursa zilizopo katika mkoa wa Pwani na kuzitangaza kupitia mwongozo wa uwekezaji ambao pia ulizindulia juzi. Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewataka wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe wanasimamia miundombinu inayoelekea kwenye viwanda vilivyopo kwenye maeneo yao.

"Kila mmoja ahakikishe maji, umeme na barabara vinafika kila eneo ambalo mwekezaji anataka kujenga kiwanda. Nitumie fursa hii kuwaomba mlete mabadiliko chanya yanayotokana na maboresho yanayofanywa na serikali."

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, alisema serikali imeanza kutekeleza mapendekezo ya mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuondoa tozo 163 zilizokuwa zikilalamikiwa na wawekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikillo, aliwataka watu wote wanaotaka kuwekeza nchini waufikirie kwanza mkoa wa Pwani kwa sababu uko kimkakati na una fursa nyingi ikiwamo hali nzuri ya usalama na kwa maana hiyo mitaji yao italindwa.

"Mkoa wetu uko kwenye eneo la kimkakati la kuwezesha biashara kwa kuwa uko karibu na Bandari ya Dar es Salaam na uwanja wa ndege; uko karibu na soko kubwa ambalo ni Dar es Salaam; unapitiwa na reli zote kwenda mikoani na nchi jirani; unapitiwa na barabara kuu itokayo Dar es Salaam na pia una bandari kavu ya Kwala."

Dk. Tausi Kida, Mkurugenzi wa Taasisi ya Uchumi ya Kijamii (ESRF) ambayo ilisimamia uandaaji wa mwongozo wa uwekezaji kwa mkoa wa Pwani, alisema taasisi yao inasaidia kuandaa na kuchambua fursa zilizopo kwenye mikoa mbalimbali. "Hadi sasa tumekwishaisaidia mikoa 17 kuandaa miongozo ya uwekezaji na kwa sasa mikoa 12 imeshakamilisha na mikoa mitano iko kwenye hatua mbalimbali," alisema.

Akitoa taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, ambao ni wadhamini wakuu, Ofisa Mkuu wa Biashara, Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts alisema:

"Benki yetu inatoa mikopo ya biashara na uwekezaji katika maeneo mbalimbali ambapo mikopo ya kilimo ni Sh. bilioni 357, uzalishaji wa viwanda (Sh. bilioni 214), biashara (Sh. bilioni 347), hoteli (Sh. bilioni 87) na sekta ya madini (Sh. bilioni 91)," alisema.

# Bodaboda wachekelea kuingizwa bima ya afya

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

UMOJA wa madereva wa bajaji na bodaboda mkoani Tabora wameipongeza serikali kwa kuwasaidia kuingia katika mfumo wa kupata huduma za matibabu kupitia bima ya afya.

Wamesema hatua hiyo itasaidia kuwapa fursa ya kuokoa maisha yao wanapopata matatizo mbalimbali ikiwamo wanapopata ajali na wakati mwingine kuugua.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa madereva najaji, Waziri Kipusi, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ya kuwahamasisha madereva bajaji na bodaboda kujiunga na bima ya afya.

Alisema kabla ya kuanza kwa utaratibu huo, walikuwa wakilazimika kusema uongo ili wenzao waliopata ajali wapate matibabu.

"Ikitokea mwenzetu amepata ajali na tunaposhindwa kuchangishana ilibidi wakati mwingine tusema uongo ili tumwokoe mwenzetu aliyepata majanga... na wakati mwingine tuliwadanganya Maofisa Ustawi wa Jamii ili watupe kibali cha kupata matibabu kwa mkopo wa matibabu," alisema.

Mwenyekiti wa umoja wa madereva bajaji mkoa, Said Maganga, alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kuwawezesha kuwa na uhakika wa kupata matibabu wakati wote na kuendelea na shughuli za kujiingizia kipato.

Mwanri aliwataka vijana wote wanaojihusisha na usafirishaji wa abiria kwa kutumia bajaji na bodaboda kuchangamkia fursa hiyo iliyotolewa kwao na serikali ya awamu ya tano.

Alisema kupitia utaratibu huo watanufaika kwa kupata huduma za bima ya afya kwa kuchangia Sh. 100,000 kwa mwaka badala ya ule wa mtu mmoja kulipa Sh. laki 1.5 kwa mwaka ili kupata huduma hizo.

Mwanri alisema serikali imeamua kuwapunguzia mzigo kwa wale bodaboda na bajaji ambao watakuwa wako katika umoja ili waweze kupata huduma za afya kwa gharama nafuu.

Naye Meneja wa Bima ya Afya Mkoa wa Tabora, Adam Salum, alisema siku za nyuma Mfuko wa Bima ya Afya ulikuwa ukihudumia watumishi wa umma pekee lakini hivi sasa umeingia makundi mbalimbali kama vile wajasiriamali, umoja wa bodaboda na bajaji.

# Waziri afagilia uwekezaji wa benki

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepongeza uwekezaji unaofanywa na Benki ya Maendeleo ya TIB kwa kuwezesha uwekezaji kwa viwanda na kampuni ya wazawa hivyo kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Pongezi hizo zilitolewa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, wakati alipotembelea banda la Benki ya Maendeleo TIB wakati wa Maonyesho ya Wiki ya Viwanda ya Mkoa wa Pwani yanayoendelea mjini Kibaha.

Mhandisi Manyanya aliyekuwa akimwakilisha Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika uzinduzi wa maonyesho hayo, alisema uwekezaji unaofanywa na TIB umechangia kwa kiasi kikubwa kuondoa utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi na kutoa ajira kwa Watanzania.

"Uwekezaji wa benki hii unasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje kama tunavyojiona bidhaa hizi zinazozalishwa hapa nchini ambazo kwa miaka mingi tulitegemea kuagiza kutoka nje ya nchi," alisema.

Naye Naibu wa Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, aliwahakikishia wazalishaji wa nyaya na vifaa vya umeme kuwa waendelee kuzalisha vifaa bora, kwa kuwa soko la bidhaa hizo lipo hasa kwa kuzingatia uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali katika sekta ya nishati.

Alisema serikali kwa makusudi imeamua kuzuia uagizaji wa bidhaa kutoka nje ambazo zinazalishwa hapa nchini ikiwamo nyaya za umeme ili kulinda viwanda vyetu vya ndani.

"Naomba niwahakikishie kuwa soko la bidhaa zenu lipo na kama mnavyofahamu serikali imezuia uingizaji wa bidhaa kutoka nje ambazo zinaweza kuzalishwa na wawekezaji wa ndani ya nchi," alisema. Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Patrick Mongella, alisema TIB ikiwa benki ya kisera, inatekeleza kwa vitendo juhudi za serikali kwa kuwezesha uwekezaji wa viwanda nchini ili kuongeza ajira na kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje.

Alisema imekuwa mwanzilishi wa miradi mipya ya kimkakati ambayo sekta binafsi haiwezi kuwekeza fedha kuanzisha miradi hiyo ikimaanisha kutoa fedha katika miradi inayoanza.

Aliongeza kuwa benki hiyo imekuwa chanzo cha kuibua mifumo mbadala na bunifu ya ugharamiaji wa maendeleo mfano matumizi ya hati fungani za Manispaa, miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi, pamoja na hati fungani za kugharamia miundombinu.

# Wakulima washauriwa kutumia chokaa mazao

**Na Enok Charles**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Kuu Kusini (Sagcot) kimewaomba wadau wa sekta ya kilimo kuwashawishi na kuwaongoza wakulima ili wapime afya ya udongo wa mashamba yao na kuongeza matumizi ya chokaa mazao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Sagcot, Geoffrey Kirenga, alisema jijini Dar es Salaam kuwa wameamua kukazania upimaji wa afya ya udongo pamoja na matumizi ya chokaa mazao ili kuongeza rutuba katika ardhi na kumepusha mkulima na matumizi makubwa ya mbolea.

Amewasihi wadau katika sekta ya kilimo nchini kukazania suala la uboreshaji wa afya ya udongo na matumizi ya chokaa katika juhudi ya sasa ya kutekeleza Mpango wa Pili wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Tanzania (ASDP II) ili kukuza uzalishaji mazao ambao ni kichocheo cha ujenzi wa viwanda.

"Chokaa mazao inapatikana katika maeneo mengi ya Tanzania. Tuwaongoze wakulima waitumie ili ardhi ipate rutuba na tuwaepushe na matumizi makubwa ya mbolea," alieleza na kuwaomba watumishi wa Sagcot na wabia nao pia kuliwekea mkazo jambo hilo.

Kirenga alisema katika ushoroba unaohudumiwa na kituo chake, licha ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuwaunganishia wakulima kupitia miundombinu ya barabara na ujenzi wa maghala katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa, taasisi hiyo lazima ikazanie kutoa elimu kwa wakulima ili kuongeza ufanisi.

"Kwa sasa hali ya miundombinu imeimarika sana, uwepo wa barabara zinazopitika, umeme pamoja na mbegu za kisasa ni kati ya maeneo ambayo tumefanikiwa sana kwa kushirikiana na wabia wetu, kazi tuliyonayo ni kumuunganisha mkulima na mnyororo wa thamani," alieleza Kirenga.

"Wengi wa wakulima wetu hawahusishi afya ya udongo na wingi wa mavuno, hawafikirii kupima ardhi kabla ya kupanda. Wadau sote tuungane kuwashawishi na kuwaongoza wakulima wapime ardhi na kuboresha afya ya udongo ili wapate mavuno mengi zaidi. Matumizi ya chokaa mazao ni muhimu katika kuboresha ardhi iliyochoka na kupunguza matumizi makubwa ya mbolea," aliongeza.

"Zipo jitihada tulizozifanya kwa kushirikiana na wabia wetu hususani katika mazao ya kimkakati ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, viazi mviringo ni mfano wa zao tulilofanyia utafiti kwa kuleta aina mbalimbali za mbegu hali ambayo imeongeza uzalishaji."

# Mhasibu, mhandisi matatani kwa tuhuma za ubadhirifu

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inawashikilia watumishi wawili, akiwamo Mhasibu wa Hospitali ya Mkoa wa Lindi (Sokoine) kwa tuhuma za makosa ya ubadhirifu wa fedha za miradi.

Kati ya miradi hiyo ni wa ujenzi wa wodi ya watoto wenye thamani ya Sh. 221,000,000.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Briedia Jenerali John Mbungo, aliyaeleza hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Wanaoshikiliwa ni mhasibu wa Hospitali ya Sokoine, Clemence Olomi na mhandisi msaidizi wa iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi (sasa Mtama), Zebedayo Seleimani.

Jenerali Mbungo alisema watumishi hao wanakabiliwa na makosa ya kufanya ubadhirifu wa Sh. 221,000,000 za miradi ya ujenzi wa wodi ya watoto, maabara na choo kwa matumizi ya wagonjwa wanaopatiwa huduma za matibabu.

Alisema makosa yanayowakabili watumishi hao ni pamoja na kuandaa nyaraka za malipo hewa yanayozidi kiwango kilichoidhinishwa kwenye mikataba iliyoingiwa na wazabuni mbalimbali, huku wakitambua kufanya hivyo ni kosa.

Jenerali Mbungo alisema watumishi hao walikamatwa Oktoba 16, mwaka huu, ukiwa ni utekelezaji wa agizo lililotolewa na Rais John Magufuli, na kuongeza kuwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi watatoa taarifa.

Aidha, aliwaomba wananchi kuunga mkono jitihada anazozifanya Rais Magufuli katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa, ikiwamo kutoa ushahidi.

Rais Magufuli akitoa agizo hilo baada ya kufunga mbio za Mwenge wa Uhuru na kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Oktoba 14 mwaka huu mkoani Lindi.



Msajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria, toka Wizara ya Katiba na Sheria, Felister Joseph Mushi, akiwasilisha mada kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria, itakayoadhimishwa kitaifa wilayani Bariadi mkoani Simiyu jana. Lengo la maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya 'Msaada wa Kisheria kwa Maendeleo Endelevu' ni kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi na utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kisheria kwa watendaji wa ngazi mbalimbali na msaada wa kisheria kwa wananchi, wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili wa kujitegemea, zikiwamo huduma za bure kwa mahabusu na wafungwa magerezani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wito wakulima kutumia ardhi ndogo

**Na Christina Haule**

WAKULIMA nchini wametakiwa kutumia ardhi ndogo ya kilimo waliyonayo kuzalisha kwa tija na kufikia malengo ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (CSA).

Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Kimataifa inayohusika na masuala ya ukanda wa kilimo (IITA), Dk. Freddy Baijukya, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari za kilimo, sayansi na teknolojia Tanzania (TAJF) jijini Dar es Salaam kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Misaada la Marekani (USAID).

Dk. Baijukya alisema, matumizi ya ardhi ndogo kwa kilimo chenye tija yatasaidia mkulima kuzalisha mazao ikiwamo mahindi kwa wastani wa tani 2 na nusu kwa hekta kiasi ambacho hakijafikiwa hata nusu yake hadi sasa.

Alisema, wamejipanga kuelimisha wakulima juu ya CSA inavyoangalia na kuondoa madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza uzalishaji wenye tija, kuzingatia uhimilivu kwenye mabadiliko ya tabianchi sambamba na kupunguza uzalishaji wa gesi za kijani ikiwamo gesi ya ukaa jambo litakalomsaidia mkulima.

Aidha, alisema, licha ya ufugaji na kilimo kuonekana kuwa ndio chanzo cha mabadiliko ya tabianchi, lakini ndio sehemu ya uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hivyo, alisema ni vema malengo na sera yaliyowekwa na serikali yaweze kutekelezeka.

Hata hivyo, alisema masuala ya CSA yanakwenda sambamba na masuala ya kuzingatia jinsia ili kumfanya mwanamke mkulima kutoachwa nyuma katika maendeleo ya kilimo nchini kama ilivyokuwa awali.

"Mfano eneo la Iringa uzalishaji wa zao la pamba umeshuka kutokana na wanawake kususa kupalilia, kwa sababu wanaume wanalala hoteli miezi mitatu baada ya mauzo na kurejea nyumbani wakiwa hawana kitu," alisema.

Dk. Baijukya alisema kumsaidia mwanamke kuendeleza kilimo kunaweza kufanikiwa kwa kuleta mashine rahisi zitakazomsaidia na hivyo kumpa nguvu ya kuendeleza kilimo nchini.

Naye Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo kitengo cha Mazingira, Evelyn Kagoma, alisema wizara imeendelea kuandaa sera na mipango mbalimbali ya kusaidia wakulima ikiwamo kufanya urutubishaji wa ardhi na upatikanaji wa maji kwenye maeneo ya kilimo.

Aliitaja mipango mingine ni kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kufuata mwongozo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi uliozinduliwa rasmi mwaka 2017.

# RC Mnyeti aridhishwa na utekelezaji wa miradi

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amefurahishwa na kasi ya wananchi wa kata za Bwawani na Matui kwa usimamizi mzuri wa fedha za serikali katika ujenzi wa madarasa ya shule wilayani Kiteto.

Akiwa katika ziara yake ya kikazi kukagua miradi na kutatua changamoto wilayani humo, Mnyeti alitembelea ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu alisema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha.

Alisema ujenzi wa madarasa pamoja na nyumba za walimu ulitekelezwa katika vijiji vya Bwawani, Kazingumu na Azimio na kila kijiji kilipokea fedha kiasi cha Sh. milioni 60, kutoka kwa mamlaka ya elimu Tanzania (TEA), kwa ajili ya kutatua changamoto ya upungufu wa madarasa.

Shule zilizopokea fedha hizo, ni Shule ya Msingi Kazimu na Azimio, ambapo shule ya msingi Azimio ilipokea kiasi cha Sh. milioni 60, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na nyumba moja ya walimu.

Shule ya Kazingum ilipewa fedha Sh. milioni 66, kutoka kwenye programu ya elimu bila malipo (EP4R). Fedha hizo, zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo, na katika Shule ya Msingi Bwawani walijenga ofisi moja ya walimu na matundu 12 ya vyoo na vyumba vitatu vya madarasa na ilipokea Sh. milioni 60.

"Niwapongeze kwa kujenga miundombinu mizuri ya gharama nafuu kwa kutumia Sh. milioni 12, kwa kila darasa na tayari madarasa yamekamilika na umeme umewekwa pamoja na gypsum kupitia fedha hizi, sehemu nyingine ujenzi huu umetekelezwa kwa gharama ya kiasi cha Sh. milioni 17, kwa kila darasa moja na bado haukukamilika," alisema Mnyeti. "Tumetembelea maeneo mengine wametumia Sh. milioni 60, kujenga madarasa mawili na fedha zimeisha bila ujenzi kukamilika, watu waliokula fedha hizo tunavyoongea watu hao wapo magereza," alisema Mnyeti.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono maeneo ambayo watakuwa na usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo huku akiwataka wananchi kuongeza nguvu kwenye miradi hiyo kwa kuchangia fedha pale zinapohitajika na siyo kutengemea fedha za serikali peke yake.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Azimio, Johnson Shirima, alisema kukamilika kwa mradi huo kumesaidia wanafunzi na walimu kupata eneo la kufundishia na kujifunzia lakini pia vyumba vya madarasa vilivyojengwa vimepunguza changamoto ya msongamano wa wanafunzi uliokuwapo mwanzo.



Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wilayani Kishapu, Suzana Masebu, akielezea changamoto wanazokumbana nazo wazee wilayani humo, yakiwamo mauaji, ukosefu wa vitambulisho vya matibabu, kwenye kikao cha Shirika la Tawlae la kutetea haki za wazee mkoani Shinyanga, wakati likitambulisha mradi wa kuhamasisha uingizwaji masuala ya wazee kwenye bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, ili kuwatatulia changamoto zao mbalimbali. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Achaguliwa bosi wa ALAT

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Sabore Kennedy Molloimet, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha, kwenye mkutano uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Arusha DC.

Akitangaza matokeo, Makamu Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha, Kalisti Lazaro ambaye ni Meya wa Jiji la Arusha, alisema uchaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa kanuni ya za kudumu za mikutano ya uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya za mwaka 2009, kifungu cha 42, 43 na 44.

Kalisti alimtangaza mwenyekiti huyo, kwa Mwenyekiti Halmashauri ya Longido, Sabore kuwa Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha baada ya kupata kura za ndio zaidi ya nusu ya kura za wajumbe walioshiriki kwenye mkutano huo.

Alisema Sabore alipata kura 21, za ndio kati ya kura 22, zilizopigwa na wajumbe, huku kura moja ikiharibika na alishinda na kupata dhamana ya kuwa Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Arusha, Sabore Molloimet, aliwashukuru wajumbe kwa kumpa dhamana ya kushika nafasi hiyo, na aliwaomba wajumbe hao, washirikiane kufanya kazi na waweke pembeni tofauti zao za kiitikadi kwa maslahi mapana ya wananchi waliowachagua na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, ameahidi kutumia uwezo alionao, kusimamia nafasi hiyo kwa haki na aliwataka wajumbe kutimiza wajibu wao pamoja na kuheshimu makubaliano na kusimamia utekelezaji wake.

"Nashukuru kwa kunipa nafasi hii na uwezo ninao, naahidi kuutumia kwa kutenda haki, na zaidi tutumie nafasi zetu kuwahudumia wananchi kwa maslahi ya wananchi," alisema Sabore.

Awali Mwenyekiti huyo, alichukua nafasi hiyo, iliyoachwa wazi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Karatu, Jubilete Mnyenye, aliyepoteza sifa za kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo.

# Watalii wapaisha mapato hadi bil. 2.3/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WATALII wanaotembelea jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori Burunge (JUHIBU) iliyopo wilayani Babati mkoani Manyara, wameongeza mapato ya jumuiya hiyo na kufikia Sh. bilioni 2.3, kwa kipindi cha mwaka 2018/19.

Spika wa jumuiya hiyo, Marcel Yona, alitoa taarifa hiyo juzi katika hafla ya kupokea udhamini wa masomo ya Chuo cha Wanyamapori Mweka wa mtoto yatima Neema Mollel, uliotolewa na Taasisi ya Chemchem Association iliyowekeza katika hifadhi hiyo.

Alisema katika mapato hayo ya mwaka, kiasi cha Sh. milioni 100.9 zimetolewa kwa kila kijiji kinachounda jumuiya hiyo, na kuna vijiji 10 vinavyounda jumuiya na kila kijiji kilipokea Sh. milioni 200, na fedha hizo zilitolewa kwenye Halmashauri ya Babati na Sh. milioni 500 zimekwenda Wizara ya Maliasili na Utalii. Alisema fedha hizo zinakusanywa katika maeneo ya wawekezaji katika hifadhi hiyo, na mwekezaji mkubwa ni Chemchem ambye anafanya utalii wa picha na hoteli za kitalii. Akizungumza baada ya kupokea udhamini wa masomo ya astashaha katika Chuo cha Wanyamapori cha Mweka, Neema Mollel, alishukuru Taasisi ya Chemchem kwa kumdhamini kumlipia ada zaidi ya Sh. milioni 7.5 kwa mwaka.

"Mimi ni yatima sina baba wala mama walifariki tangu mwaka 2005, nimekuwa nikisoma kwa ufadhili hadi kidato cha sita, na sasa nashukuru Chemchem kwa msaada huu mkubwa katika maisha yangu," alisema Neema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Chemchem, Walter Pallangyo, alisema taasisi hiyo imeamua kumdhamini masomo mwanafunzi huyo kama sehemu ya mchango wake katika jamii.

Pallangyo alisema sambamba na mwanafunzi huyo, pia taasisi hiyo imewadhamini masomo wanafunzi wengine wanaoishi ndani ya JUHIBU WMA katika vyuo vya ufundi, masuala ya Utalii na Sekondari. "Tunaomba jamii hii iendelee kuhifadhi wanyamapori na mazingira ili tuendelee kupata watalii zaidi ambao ndio wanaleta fedha ambazo zinasaidia kusomesha watoto, ujenzi wa shule, vituo vya afya na miradi mbali mbali ya wananchi," alisema

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Minjingu Godfrey Sailale, alisema mchango wa wawekezaji katika sekta ya utalii katika hifadhi ya wanyamapori ya Burunge umeongezeka sana na sasa wananchi wanaona umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kupiga vita ujangili.

"Uhifadhi katika eneo hili umekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii, kwani tumejengewa shule na Chemchem, wametoa madawati, vitabu katika shule na kusaidia miradi mingi ya jamii," alisema. Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Burunge(JUHIBU) ilianzishwa mwaka 2003, inaundwa na vijiji 10, ambavyo ni Sangawe, Mwada, Ngoley, Vilimavitatu, Minjingu, Kakoi, Olasiti, Manyara, Magala na Maweni na ina ukubwa wa 283.

# Siha yatarajia nuru mpya kupambana ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

UTASHI wa kisiasa wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kuruhusu wadau wa maendeleo kushughulika moja kwa moja na tatizo la ukatili dhidi ya watoto wa kike kwenye Kata za Sanya Juu, Nassai na Livishi, unatajwa huenda ukaleta 'nuru' mpya katika kupambana na uhalifu huo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Juma Jani, alisema utashi wa kisiasa kwa sasa ni muhimu katika kupambana na vitendo hivyo, huku akiwasihi wanasiasa wengine kutoa ushirikiano kwa asasi za kiraia kutimiza wajibu wake.

Alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi wa mradi wa kujengea jamii hamasa kuhusu uwapo wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili hususani dhidi ya watoto wa kike katika wilaya hiyo.


"Uongozi wa kuacha alama ni pamoja na uwekezaji katika huduma za kijamii ambazo ndizo zinachangia kwa kiasi kikubwa kutimiza malengo ya maendeleo ya wilaya yetu. Hatuna sababu za kuukwepa mradi huu, sisi tunawakaribisha na tumeupokea ili mtusaidie kutoa elimu kwa umma. Tunajua hauwezi kuiangusha halmashauri ila unakuja kujenga na tunaamini tutawanusuru watoto wa kike na ukatili unaoendelea," alisema Jani, Diwani wa Kata ya Sanya Juu.

Mradi huo wa miezi minane unaotekelezwa na Shirika la Kwieco, kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society, utazihusisha shule 12 ambazo zitaundwa vilabu vya kupinga ukatili huo.

"Kwa kuwa sisi ni waathirika wakubwa wa ukatili dhidi ya watoto wa kike, niwaombe mtusaidie kuishawishi serikali na hasa Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro (RAS), iharakishe Siha nayo iwe na kituo jumuishi cha pamoja (One stop centre).

Akijibu ombi hilo, Mratibu wa mradi huo, Peter Mashingia, alisema kituo hicho ambacho kinapaswa kuwekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Siha, ni muhimu kwa ajili ya huduma za uchunguzi kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia ambao watapelekwa hapo katika muda usiozidi saa 72 baada ya tukio la ukatili na kupatiwa bure huduma.

Kwa mujibu wa Mashingia, matarajio yao kutokana na mradi huo ni kuona waathirika wa ukatili wanapata huduma za haraka, za ubora na kwa wakati huku washukiwa wakichukuliwa hatua ili jamii iendelee kuimarisha imani katika uwajibikaji wa vyombo husika. Taarifa ya Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Siha, Peter Msaka, ilieleza kuwa kundi hilo la watoto wa kike lililopo katika mazingira hatarishi, litakapojengewa uwezo, litapata ujasiri wa kutoa ushuhuda ya namna walivyookolewa katika vitendo vya ukatili wa kijinsia na uhalisia wa viongozi katika kushughulikia matukio hayo.



Mkuu wa Kitengo cha Elimu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Faith Shayo (kulia) na Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Shule wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mathias Mvula (kushoto), wakiwaangalia baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Kwamwande iliyopo Kilindi mkoani Tanga, walipokuwa wakitumia vishkwambi viliyotolewa na XPRIZE kupitia Unesco kwa ajili ya kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia ubunifu wa teknolojia wakati wa hafla fupi ya kukabidhi vishkwambi hivyo, iliyofanyika mwishoni mwa wiki shuleni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miti Mlima Kilimanjaro kulindwa kitaalamu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATAALAMU wa mazingira wameanzisha mpango wa kuilinda miti inayooteshwa katika Mlima wa Kilimanjaro kwa kutumia kifaa maalumu cha kukokotoa mawasiliano ya kijiografia (GPS).

Kuanzia sasa, miti yote iliyooteshwa na inayooteshwa na wananchi au taasisi mbalimbali ili kuilinda ikolojia na theluji ya Mlima Kilimanjaro isipungue, itafuatiliwa kwa kutumia kifaa hicho.

Jana, mkuu wa kitengo cha usimamizi wa miti kwa njia ya mtandao kutoka Shirika lisilo la kiserikali la 'The Kilimanjaro Project', Samwel Andrew, akizungumza wakati wa upandaji miti katika Shule ya Sekondari ya Kimochi, Moshi Vijijini, alisema mpango huo unapatikana kwenye programu ya play store.

GPS ni mfumo unaotumika kukokotoa mahali mtu au kitu au kifaa hicho kipo kwenye sehemu yoyote duniani.

"Kwa sasa tumeanzisha programu hiyo ili kuhakikisha miti yote inayopandwa haifi hata mmoja. Programu hii inapatikana kwenye play store, lakini ili kuitumia lazima uje kwetu tuweze kukupa maelekezo ya namna ya kutumia, kwa sababu unapaswa kupiga picha mti mmoja mmoja, na sio yote kwa ujumla.

"Hii ni fursa kwa wananchi kwa kila atakayeingiza mti wake kwenye mtandao huo na kuufuatilia ipasavyo atalipwa Shillingi 100 kwa kila mti. Tunalenga kuwahamasisha Watanzania kupanda miti zaidi na kuitunza bila kutoa sababu za visingizio."

Ofisa uhamasishaji wa Shirika mwenza la Nipe Fagio, Wilyhard Shishikaye, alisema katika Shule ya Sekondari Kimochi, wameshaotesha miti 250 ya aina tano tofauti, ikiwamo miti ya asili ya mikuyu na mizambarau.

Pia alisema wanatoa elimu ya namna ya kuotesha miti na maeneo ya kuotesha ili kulinda uoto wa asili na kutunza mazingira kuzunguka Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Kutokana na ujio wa mpango huo, Mkuu wa Shule hiyo, Crispin Nyoni, aliishukuru taasisi hiyo kwa kujitokeza kutoa elimu kwa wanafunzi na wananchi wa vijiji jirani kuotesha miti hiyo ya asili.

Mwezi Juni mwaka 2018, theluji ya Mlima Kilimanjaro iliongezeka kwa sentimita 33.6 kwa kupindi cha miezi mitatu iliyoishia Machi. Ongezeko hilo inaelezwa kwamba linatokana na mvua kwenye kilele cha mlima huo.

# Vijana watakiwa kuzibana h'shauri kupata mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

VIJANA zaidi ya 300 waliokuwa wakishiriki elimu ya ujasiriamali kuelekea maendeleo endelevu ya Tanzania ya viwanda wametakiwa kuacha kulalamika kutopata ajira, badala yake wazibane halmashauri za wilaya kutoa kwa wakati mikopo ya asilimia 10 inayotengwa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hoja ya kutaka vijana wazibane halmashauri zinazochelewa fedha hizo kuzitoa, ilitolewa jana mjini Moshi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Sophia Islamic Foundation (SIF), Sofia Said.

"Serikali haiwezi kuajiri watu wote kwa wakati mmoja, ndiyo maana imeamua kutenga asilimia 10 ya mapato katika kila halmashauri kwa ajili ya mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Na serikali yetu haina dini, ndiyo maana inatoa mikopo kwa vijana wote waliojiunga kwenye vikundi ili waweze kujiajiri wenyewe, changamkieni na mzibane halmashauri ambazo hazitengi fungu hili," alisisitiza.


Aliwaeleza vijana hao kwamba wanachotakiwa kukifanya kwa sasa ni kujiingiza katika sekta isiyo rasmi hasa ujasiriamali ambao ni mtazamo wa akili ya mtu katika kutafuta fursa, kuwa tayari kukabiliana na matatizo na kuwa na uwezo wa kutengeneza faida, kwa kuanzisha ama biashara mpya au kuongeza tija katika taasisi.

Dhana ya ujasiriamali ina tafsiri pana, lakini hujumuisha shughuli nyingi ikiwa ni pamoja na kuwa na wazo, kutengeneza na kuendesha biashara.

"Unajua ujasiriamali unajumuisha ubunifu, kutengeneza kitu kipya na kuwa tayari kukabiliana na ugumu, vilevile kuwa na uwezo wa kupanga na kuendeleza miradi ili kufikia malengo, ndiyo maana tukawaleta hapa tuwafundishe kujitegemea kibiashara na kuacha kulalamika kila siku, huku mkisubiri tu ajira serikalini," alieleza mkurugenzi huyo.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa Kiislam mkoani Kilimanjaro, Idrissa Muro, akizungumza kuhusu ujasiriamali, alisema elimu waliyoipata itawasaidia kuinua kipato chao na kuachana na utegemezi.

Nipashe Spoti



JUVENTUS WAKIFANYA HIVI VITATU WATASHINDA UEFA UK. 20



## ISIKUPITE

MABOSI wa Manchester City wanajiandaa kumpa mkataba mpya wa pauni 450,000 kwa wiki mshambuliaji wao, Raheem Sterling, ili kujilinda isimpoteze nyota huyo. Real Madrid imeweka wazi nia yake ya kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England, ambaye ana umri wa miaka 24.

# JUU KWA JUU

Beki wa kati wa Barcelona, Samuel Umtiti (juu), akipambana kuwania mpira na mchezaji wa Eibar katika mechi ya La Liga iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Manispaa ya Ipurua. Barca ilishinda mabao 3-0 na kufikisha pointi 19 na kujiimarisha kileleni katika msimamo wa ligi hiyo. **PICHA:**

SOKA



# SABABU 4 LIVER KUTWAA TAJI EPL MSIMU HUU

**LONDON,** England

MBIO za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu zinaendelea na kwa hakika zinavutia.

**Baada ya mechi nane (kabla ya mechi za juzi na jana), klabu moja inaonekana kuwa kwenye mbio kasi zaidi kuliko nyingine.**

Kutabiri nani mshindi wa taji la Ligi Kuu England mara zote inakuwa ngumu, lakini msimu huu inaonekana kama vile inaweza kuwa rahisi.

Wote tunaweza kukubali kwamba, Liverpool wapo kwenye nafasi nzuri zaidi kutokana na kuonyesha kiwango cha kuvutia.

Msimu uliopita kulikuwa na ushindani mkubwa kwenye mbio hizi kati ya wekundu hao na Manchester City. Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kilipata pointi za rekodi wakati kikifikisha pointi 97, lakini kilikosa taji hilo kwa tofauti ya pointi moja tu dhidi ya City.

Baada ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool sasa inaonekana kwamba imekamia kulitwaa taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Makala hii inakuchambulia sababu nne kwanini vijana hao wa pale Merseysiders msimu huu wanaweza kuweka historia ya kulitwaa taji hilo.

### 4 MWANZO MZURI

Liverpool inaonekana ni timu iliyojipanga zaidi kwenye ligi hiyo msimu huu, hasa kutokana na matokeo yake ya mwanzo kabisa. Wakati timu nyingine zimepoteza pointi zake, wekundu hao wameweza kuwa na mwanzo mzuri wa msimu kwa kupata asilimia 100 ya matokeo na inaonekana wazi kwamba hawaonekana kama watapunguza kasi.

Kwa sasa wana safu ya ulinzi bora zaidi, wakiwa wameruhusu kufungwa mabao sita tu katika mechi nane, wakicheza mechi mbili bila kuruhusu bao. Wana safu bora ya ushambuliaji, hadi sasa ikiwa imefunga jumla ya mabao 20 yaliyofungwa na Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino.

Vijana hao wa Klopp wanaonekana wazi kwamba, kasi yao haizuiliki msimu huu kwenye mbio za ubingwa.

### 3 KUSHUKA KWA MANCHESTER CITY

Tangu Pep Guardiola alipoondoka pale Bayern Munich na kuchukua changamoto mpya kwenye Ligi Kuu England, Manchester City mara zote imekuwa ikiwekwa kama moja ya timu inayopewa nafasi kubwa zaidi ya kutwaa taji la Ligi Kuu. Baada ya ushindi mfululizo, inaonekana kama msimu huu mambo magumu kwao.

Baada ya kushuhudia mechi nane za Ligi Kuu, wengi wanatabiri kwamba, msimu huu hataweza kulitwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo. Hiyo ni kwa sababu ya kushindwa kuwa na mwendelezo wa kiwango bora na kuwaruhusu Liverpool kutangulia mbele yao.

Kiukweli inaweza kuwa ni mapema mno kutabiri mshindi wa ligi katika hatua hii, lakini dalili zinaonyesha kwamba mambo kwa upande wa City hayako sawa. Lakini bila shaka City inabakia kuwa timu ambayo inatoa ushindani mkubwa kwa Liverpool.

Katika mechi nane msimu huu hadi sasa, vijana hao wa Guardiola wameshinda mechi tano, sare moja na vipigo viwili. Hii imewaacha kuwa na pointi 16. Katika upande mwingine, Liverpool wao wana pointi 24.

### 2 KIPAUMBELE CHA LIVERPOOL TAJI EPL

Mashabiki wa Liverpool wanaweza kuota tena. Hii ni kutokana na vijana hao wa Klopp kuwa na ndoto kubwa ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30.

Kwa mara ya mwisho Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England ilikuwa ni msimu wa 1989-90 chini ya utawala wa Kenny Dalgish. Tangu wakati huo, mashabiki wake wameshuhudia klabu kama Chelsea, Arsenal, Manchester United, Manchester City na Leicester wakilibeba taji hilo.

Msimu uliopita ilikaribia kulibeba taji hilo, lakini tofauti ya pointi moja ikalifanya taji hilo kwenda kwa Manchester City. Hata kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya halikutosha kwao kuweza kuwafidia mashabiki wao ambao tayari walijiandaa kwa taji hilo.

Baada ya hilo, sasa vijana hao wa pale Merseysiders nia yao msimu huu ni moja tu - kulitwaa taji la Ligi Kuu. Wamejipanga kweli kweli ili kuhakikisha kwamba wanaondoka na taji hilo.

Mwanzo wao wa asilimia 100 msimu huu umewafanya kuonekana kuwa wapo kwenye mbio bora kabisa kuelekea kwenye ubingwa huo.

### 1 TIMU IMEIMARIKA

Jurgen Klopp aliondoka Borussia Dortmund kuchukua nafasi ya kuinoa Liverpool kipindi cha majira ya joto mwaka 2015. Tangu hapo, Mjerumani huyo ameilinda klabu hiyo na kuifanya kuwa imara zaidi. Wekundu hao wameifanya timu hiyo kuwa kwenye daraja la juu kabisa.

Tangu mwanzo wake hapo, kulikuwa na mabadiliko makubwa ya kiwango hapo Merseysiders. Walionyesha tofauti na walivyokuwa chini ya kocha, Bredgan Rogers.

Tangu mwaka huo, Liverpool imeonekana kusonga mbele. Wachezaji wameimarika pamoja kwa kutengeneza uwiano mzuri wa kikosi ambao ulikuwa ukihitajika. Wameonyesha kubadilika kwa kiwango kikubwa zaidi.

Kocha amesajili wachezaji wengi ambao wapo kwenye kiwango bora na wa daraja la juu kabisa. Kila upande wa timu kwa sasa unaonekana umeimarika vya kutosha. Wachezaji wamekuwa pamoja na tayari kutengeneza historia mpya kwenye Ligi Kuu.

**JE, WAJUA?**



NAHODHA wa kwanza mweusi wa Timu ya Taifa ya England, Paul Ince, amesema kuwa angewaongoza wachezaji wenzake kutoka nje ya uwanja kama angekuwa katika mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Bulgaria ambayo ilikuwa na vitendo vya kibaguzi kutoka kwa mashabiki.

MICHEZO



Kiungo wa kimataifa wa Simba raia wa Sudan, Sharaf Eldin Shiboub, akifunga bao pekee kwenye mechi ya kirafiki kati ya timu hiyo dhidi ya Mashujaa Kigoma kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika wiki iliyopita. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA YACHEZA MECHI 19 BILA KUPOTEZA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, imeweka rekodi ya kucheza mechi 19 mfululizo bila kupoteza mchezo hata mmoja, tangu msimu uliopita.

**Jumatano iliyopita, timu hiyo ilifikisha mechi ya 19 kwa kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Mabingwa wa Burundi, Aigle Noir kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na kuifanya timu hiyo kucheza idadi hiyo ya michezo ikishinda tisa na kutoka sare michezo sita.**

Mechi hizo zinajumuisha michuano ya kimataifa, Ligi Kuu Bara na mechi za kirafiki za ndani na za kimataifa, zikiwamo zile za maandalizi ya msimu mpya.

Mara ya mwisho Simba kufungwa ilikuwa ni Mei 10, mwaka huu, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, msimu uliopita, kwa bao la kujifunga la Mohammed Hussein 'Zimbwe jr'.

**1. LIGI KUU MSIMU ULIOPITA**

Baada ya kipigo hicho dhidi ya Kagera Sugar, Simba iliendelea na michezo ya Ligi Kuu na safari yake ya kucheza mechi 19 ilianza ilipotoka sare ya bila kufungana dhidi ya Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita.

Mechi nyingine za Ligi Kuu msimu uliopita ni pale ilipopata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, kabla ya kuibamiza Ndanda mabao 2-0.

Ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Biashara kabla ya kumalizia mechi yake ya Ligi Kuu msimu uliopita kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro ilipotoka sare ya bila kufungana dhidi ya Mtibwa Sugar.

Tayari mpaka hapo Simba ilikuwa imeshacheza mechi tano bila kupoteza.

**2. MECHI ZA MAANDALIZI YA MSIMU**

Simba ilikwenda nchini Afrika Kusini kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu 2019/20, pamoja na mechi za kirafiki za kimataifa.

Pamoja na kufanya mazoezi ya kujenga miili, lakini pia ilicheza mechi nne za kirafiki. Ilikuwa ni mwezi Julai mwaka huu. Mechi ya kwanza ilicheza dhidi ya Orbret Tvet na kushinda mabao 4-0, kabla ya kupambana na Platinum Stars, pia ya Afrika Kusini ikaichapa mabao 4-1.

Mechi iliyofuata Simba ilicheza dhidi ya Township Rollers ya Botswana ambayo nayo ilikuwa nchini humo kwa maandalizi ya msimu mpya na timu hizo zote zilitoka sare ya kufungana bao 1-1, kabla ya mechi ya mwisho kucheza dhidi ya Orlando Pirates, pia timu zote zilitoka sare ya kufungana bao 1-1.

Hiyo ilikuwa ni mechi ya tisa kwa Simba kucheza bila kupoteza.

Ikumbukwe kuwa Township Rollers baadaye ilicheza na Yanga kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa kwa jumla ya mabao 2-1, ikitoka sare ya bao 1-1 ugenini na kufungwa bao 1-0 nyumbani.

**3. TAMASHA LA SIMBA DAY**

Lilikuwa ni tamasha la kila mwaka la Simba Day na msimu huu, ilicheza na timu ya Power Dynamos kutoka Zambia.

Katika mechi hiyo, Simba ilishinda mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Taifa na kuwa ni mechi ya 10 kwa timu hiyo kucheza bila kupoteza tangu Mei 10, mwaka huu.

**4. LIGI YA MABINGWA AFRIKA**

Simba ikaingia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika.

Ikacheza mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji na kutoka sare ya bila kufungana mechi ya kwanza na mechi pili ikawa sare ya bao 1-1.

Kwa matokeo hayo timu hiyo ilitolewa kwenye michuano hiyo kwa goli la ugenini, lakini ikaendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi hiyo na kuwa ni ya 12.

**5. LIGI KUU MSIMU HUU**

Msimu huu wa ligi, Simba imecheza mechi nne hadi sasa. Mechi ya kwanza iliichapa JKT Tanzania bao mabao 3-1, na iliyofuata ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Baada ya hapo ilisafiri hadi mjini Bukoba kwenye Uwanja wa Kaitaba, ikatoa kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar kabla ya kwenda kucheza dhidi ya Biashara United ya Mara na kushinda kwa mabao 2-0. Mpaka hapo tayari ikawa imeshacheza mechi ya 16 bila kupoteza.

**6. MECHI ZA KIRAFIKI**

Kwenye mechi za kirafiki, Simba ilicheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya Bandari ya Kenya ikashinda bao 1-0, kabla ya kutoka sare ya bila kufungana na Aigle Noir ya Burundi, huku ikiifunga Mashujaa ya Kigoma goli 1-0 kwenye mechi ya kirafiki isiyo ya kimataifa.

Hadi hapo tayari Simba ikawa imecheza mechi 19 bila kupoteza hata moja.

NJE YA UWANJA

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amekuwa njia panda kuhusu kufanya uamuzi wa kuendelea kuifundisha klabu ya Azam FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara au kusaini mkataba wa jumla wa kuinoa Stars.



# DAKIKA 45 ZA STARS KUPINDUA MEZA SUDAN



**Na Somoe Ng'itu,** aliyekuwa SUDAN

TUTASHINDA, hiyo ndiyo ilikuwa kauli ya balozi wa Tanzania aliyeko Sudan, Islima Kombo Haji, kuelekea mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

**Fainali hizo zinazoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zinatarajiwa kufanyika Februari mwakani, huko nchini Cameroon.**

Balozi huyo wa Tanzania, alikuwa akisema neno hilo moja tu la Tutashinda, kila alipokuwa akizungumza na wachezaji, viongozi, waandishi wa habari, wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma kozi mbalimbali na Watanzania wote waliokuwa jijini Khartoum, tayari kuelekea kwenye Uwanja wa El Merreikh, Omdurman ili kushuhudia mechi hiyo.

Kiongozi huyo alikuwa akiongeza hamasa kwa wachezaji, huku akiwataka wasahau kichapo cha bao 1-0 walichokipata wakiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Ushindi wa mabao 2-1, ulitosha kuwapa Taifa Stars, tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili, tena ikirudia ilichofanya mwaka 2018 kwa kuwaondoa wapinzani hao hao, Sudan, kwenye ardhi ya nchi yao.

Ilikuwa ni Ijumaa ya Oktoba 18, mwaka huu, Taifa Stars ilipofanikiwa kufuzu kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili, mara ya kwanza ikiwa ni mwaka 2008 (mwaka wa kwanza wa fainali kuchezwa), chini ya Mbrazil Marcio Maximo.

### WACHEZAJI WALA KIAPO

Siku moja kabla ya mchezo huo wa marudiano, wachezaji wa Taifa Stars wakiwa chini ya kipa mkongwe, Juma Kaseja, ambao waliweka kambi katika hoteli nzuri ya kifahari iitwayo Grand Villa, ikitizama Mto Nile, walifanya kikao chao kwa ajili ya kupanga mikakati kuelekea mchezo huo.

Kikao hicho walikipanga wachezaji wenyewe, wakiwa na malengo ya kujipanga kuhakikisha wanaingia uwanjani kwa ajili ya kuipigania nchi yao katika mchezo huo muhimu.

Katika kikao hicho, inaelezwa kwamba walikubaliana kuhakikisha wanaandika historia nyingine ya kutinga fainali hizo, kwa sababu uwezo wa kufanya hivyo wanao.

"Tumekutana, tumezungumza sana, na kikubwa kila mmoja wetu atakayepata nafasi, amekubali kupambana, kupigana na kutumia uwezo wake wote ili kuipa timu matokeo mazuri, tunaamini tunaweza, nafasi ni yetu ya kufanya kile tulichokubaliana," nahodha msaidizi wa Taifa Stars, Erasto Nyoni, aliiambia Nipashe, siku moja kabla ya mechi hiyo.

Nyoni alisema kuwa tulikubaliana kuingia uwanjani tukiwa tumesahau matokeo ya mchezo uliopita, lakini tukisema tunahitaji ushindi tu, licha ya kwamba soka lina matokeo ya aina tatu.

"Tulisema tumepata nafasi hii kwa kuaminiwa, ni lazima tuonyeshe makocha wetu waliotupa nafasi hii hawakukosea," alimaliza beki huyo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam.

Ikitokea nyuma, Taifa Stars ilianza kipindi cha pili ikiwa na kasi ya juu, baada ya kufahamu kwamba wanahitaji mabao tu, ili ndoto zao ziweze kutimia.

Walienda mapumziko wakiwa nyuma kwa bao 1-0, ikiwa na maana tayari wenyeji wao, Sudan wanaongoza magoli 2-0.

Moja ya mawaidha waliyopewa wachezaji hao ni kumwachia beki mkongwe, Nyoni, kupiga mipira ya faulo endapo itapatikana, tofauti na ilivyokuwa katika dakika 45 za kipindi cha kwanza.

"Nyoni, unawaachia vipi watoto wapige faulo, hii ni kazi yako," ni moja ya maneno yaliyozungumzwa katika chumba cha kupumzikia cha Taifa Stars na maneno hayo yalitimia kwa beki huyo, kufunga bao la kusawazisha, kabla ya mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi kufunga goli lililowanyamazisha Wasudan ambao walikuwa wameamini tayari timu yao imeshakata tiketi ya kushirii fainali za CHAN hapo mwakani.

VAN DIJK

### NDAYIRAGIJE "NABII MPYA"

Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, ameonekana kuwa ni nabii ambaye anaweza kuifikisha mbali Tanzania endapo Shirikisho la Soka Nchini (TFF), itaamua kumpa rasmi mkataba wa kuiongoza timu hiyo.

Akiwa na muda wa miezi mitatu katika kikosi hicho, Ndayiragije, amecheza mechi sita, kati ya hizo, amefungwa mchezo mmoja.

Mrundi huyo ambaye TFF ilimwazima kutoka katika klabu ya Azam FC, amefanikiwa kuiondoa Kenya (Harambee Stars) na Sudan kwenye michuano ya CHAN.

Pia kocha huyo aliyeonekana kwamba bado hataweza kufanya majukumu yake vizuri kutokana na kuhitajika pia na waajiri wake wa kila siku (Azam), aliwaondoa Warundi wenzake katika mechi za kuwania tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Dunia.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Bujumburua, Stars ililazimishwa sare ya bao 1-1, na wenyeji, na ilipowakaribisha Dar es Salaam, dakika 90 zilimalizika kwa kila upande kushindwa kutingisha nyavu za mwenzake. Lakini walipokwenda hatua ya matuta, Stars ilisonga mbele kwa kuwafunga wageni hao penalti 3-0.

"Ninaweza kumudu kazi zote mbili, ninajua namna ya kujipanga," alisema kwa kifupi Ndayiragije baada ya kuwapo kwa fununu za kutakiwa kuiacha Azam FC na kuweka nguvu zote katika kikosi cha Stars.

Kocha huyo ambaye alianza kung'ara akiwa na Mbao FC ya Mwanza na baadaye KMC ya jijini, amepokea mikoba ya kuinoa Stars kutoka kwa Mnigeria Emmanuel Amunike, ambaye naye aliweka rekodi ya kuipeleka Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), ikiwa ni baada ya miaka 39.

### MASHUJAA WAREJEA

Kikosi cha Stars, kilirejea nchini Jumamosi mchana na kupokelewa mashabiki, wadau mbalimbali wa timu hiyo pamoja na viongozi wa TFF, akiwamo Rais, Wallace Karia na Katibu Mkuu, Wilfred Kidao.

Akizungumza baada ya kuwapokea "mashujaa" hao, Karia, alisema kuwa mafanikio yaliyopatikana ni ya Watanzania wote na wanawapongeza wachezaji kwa kupambana kuhakikisha wanapata ushindi.

Karia alisema kuwa hawatabweteka na sasa wanajipanga kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mashindano mengine ya kimataifa kwa sababu nia yao ni kuona wanafuzu michuano mbalimbali.

"Hongera sote, ni hongera ya Watanzania wote, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ameona jitihada zetu, ameona jitihada zetu, zilizo bila hila, tuko katika ulimwengu wa mpira, ukimaliza hili, linakuja lingine, tunajipanga mengine yanayokuja ili tufanye vizuri katika mashindano mengine, hatujafika, hatutabweteka," alisema Karia. Aliongeza kwamba tunatakiwa kuweka misingi imara ili kufikia malengo huku akisema kuwa uongozi wake unajivunia alama ambayo itabakia.

"Najisikia vizuri, tumepata nafasi nyingine ya kushiriki mashindano makubwa,

Chini ya uongozi wa Karia, ambao una miaka miwili, Taifa Stars imefanikiwa kushiriki fainali za Afcon na CHAN.

### KASEJA AFUNGUKA

Kipa huyo mkongwe ambaye sasa anaichezea KMC FC, alisema kuwa ushindi huu ni wa wote na anaamini Taifa Stars inaweza kufika mbali zaidi katika kila mashindano wanayoshiriki.

Kaseja alisema kuwa, kikubwa ni kuendelea kushirikiana kuanzia katika hatua ya maandalizi na si kusubiri matunda.

"Lengo la Watanzania lilikuwa ni kuona Tanzania tunaenda kucheza fainali za CHAN, kulikuwa na kauli mbiu kuwa Tunakanyaga Mpaka Chan,...siku zote makocha ni wengi sana, lakini benchi la ufundi linakuwa na mbinu zake, benchi la ufundi lilitupa mbinu na vile tulivyocheza ndio ilikuwa mipango ya benchi ya ufundi," alisema Kaseja.

Kipa huyo aliongeza kuwa ili Tanzania iweze kufanya vizuri zaidi katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, ni lazima idadi ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa ughaibuni iongezeke.

Alisema kuwa Taifa Stars inapokuwa na wachezaji wengi wanaocheza nje ya Tanzania, inakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupata matokeo chanya tofauti na ilivyo sasa.

"Natamani kuona Taifa Stars inakuwa na kina Mbwana Samatta watano, Simon Msuva wanne na Himid Mao wawili, tukipata wachezaji wengi wanaocheza nje, kikosi chetu kitakuwa imara, wachezaji watakuwa na uwezo wa kupambana na timu za nje, ndio jambo linalotusumbua leo hii tukikutana na timu kama Senegal," alisema Kaseja.

### CECAFA YANG'ARA

Hadi kufikia juzi jioni, timu tatu kutoka katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kati ya nane zilikuwa zimefuzu tiketi ya kushiriki fainali hizo za CHAN.

Timu hizo ni pamoja na Taifa Stars (Tanzania), Rwanda (Amavubi) na The Cranes ya Uganda. Nchi nyingine ni pamoja na Zambia (Chipolopolo), Namibia, Togo na Morocco.

## Nukuu


"Katika wiki mbili ama tatu zilizopita, ameimarika katika mazoezi. Ni vizuri. Sikufunga naye uwezekano wa kucheza. Kama yupo vizuri, kama yupo tayari, kama anapatikana na kujifua, kutupa hisia nzuri kila siku katika mazoezi, anaweza kucheza. Wazo langu ni kumtumia kila mchezaji mmoja kikosini ambaye anaweza kutusaidia. Ana uelewa mkubwa na ubora, tutamhitaji katika mechi zijazo. Ni mwenye furaha sana kwa namna anavyoimarika, Ninajisikia vizuri naye," **Kocha wa Arsenal, Unai Emery akimzungumzia Mesut Ozil**




"Si kwamba ni yeyote tu anaweza kufikia idadi hii, shukrani kwa wachezaji wenzangu na makocha ambao wamenisaidia kuwa mchezaji kama nilivyo. Ni rekodi kiasi gani nilizonazo? Sijui. Rekodi inakuja moja kwa moja - sikwenda kuzitafuta, rekodi zinanitafuta! Bila kuwa na umakini hufanyika kawaida," **Cristiano Ronaldo akizungumzia rekodi yake ya kufikisha mabao 700 tangu aanze kucheza soka.**



"Nimepata bahati ya kukutana na matukio mengi makubwa mazuri, bado kipindi cha [Pep] Guardiola nilikuwa mmoja wa wachezaji bora. Kila mwaka nimekuwa nikipambana kuongeza ubora, nafikiri ni wakati wa Guardiola, ndipo nilipokua sana kisoka wakati huo," **Lionel Messi.**





LEWANDOWSKI

# FOWADI WA5 WALIOANZA MSIMU KWA MAANGAMIZI

**LONDON,** England

BAADA ya kipindi cha usajili, msimu mpya wa ligi za soka za Ulaya umeendelea huku kila klabu ikionyesha na kutumia 'silaha' zake.

**Hadi sasa mechi nane (kabla ya juzi na jana) zimechezwa kwenye Ligi Kuu England na saba kwenye Ligi Kuu Hispania, La Liga, pia saba kwa Ligi ya Ujerumani maarufu Bundesliga na tisa zimepigwa kule kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, na Ufaransa, Ligue 1.**

Makala hii inawaangalia washambuliaji watano ambao wameanza vizuri zaidi msimu huu kwa kufunga mabao katika mashindano yote waliyoshiriki:

**5. CIRO IMMOBILE**

Nyota wa SS Lazio, Ciro Immobile kwa sasa ndiye anatamba kwenye Serie A. Mshambuliaji huyu amekuwa nguzo muhimu zaidi ya mabao kwa kikosi chake. Kwa sasa ndiye anayeongoza kwa kuzifumania nyavu kwenye Serie A.

Immobile ameichezea mechi nane Lazio msimu huu, huku saba akicheza kwenye Serie A na mchezo mmoja kwenye Ligi ya Europa. Katika mechi zote nane, Mtaliano huyo amefunga mabao nane, saba kwenye ligi na moja kwenye Ligi ya Europa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amecheza dakika 607 kwa Lazio katika mashindano yote msimu huu. Ana wastani wa kufunga bao moja katika kila mechi.

**4. VICTOR OSIMHEN**

Victor Osimhen ni mchezaji ambaye amejibainisha mwenyewe kwamba ana jicho zuri zaidi la goli. Msimu ndio kwanza umeanza na mshambuliaji huyu ameonekana kasi yake haiwezi kuzuilika.

LOSC Lille watakuwa na kazi ya ziada kumbakisha kwenye kikosi chao kama ataendelea kuwa kwenye kiwango alichonacho sasa. Amecheza mechi 11 kwa miamba hao wa Ufaransa, tisa kwenye Ligue 1 na moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Katika mechi zote amefunga mabao saba kwa jina lake. Na tayari amefunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati alipofunga dhidi ya Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Nigeria amejipambanua yeye mwenyewe kama mmoja wa wafungaji bora zaidi kwa sasa. Anaongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligue 1. Kama ataendelea kuwa kwenye kiwango chake cha sasa, hakuna anayeweza kutabiri nini kitatokea mwishoni mwa msimu.

**3. SERGIO KUN AGUERO**

Sergio Aguero alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa Manchester City wakati wanatetea ubingwa wao msimu uliopita. Kiukweli ingekuwa vigumu kwa City kufanikiwa bila mabao yake. Pamoja na kwamba City msimu huu imeanza vibaya, lakini hilo halijamwathiri raia huyo wa Argentina kuendelea kufunga. Bado ana kasi ile ile ya kufunga mabao.

Kwa sasa, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 31 analingana kwa idadi ya mabao aliyofunga na Tammy Abraham na wanaongoza kwa kufikisha mabao nane baada ya mechi nane za Ligi Kuu. Ingawa bado hajafunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, amekuwa na kasi nzuri zaidi kwenye Ligi Kuu.

**2. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG**

Pierre-Emerick Aubameyang alikuwa mmoja wa washambuliaji walioshinda kiatu cha dhdhabu kwa kufunga mabao 22 msimu uliopita. Alilingana idadi hiyo ya mabao na Mohamed Salah na Sadio Mane.

Msimu huu pia inaonyesha Aubameyang kasi yake haijapungua. Hadi sasa raia huyo wa Gabon ameicheza mechi 10 Arsenal kwenye mashindano yote. Nane kati ya hizo amecheza kwenye Ligi Kuu England na mbili kwenye Ligi ya Europa.

Aubameyang amefunga mabao nane hadi sasa, saba kati ya hayo amefunga kwenye Ligi Kuu England na moja kwenye Ligi ya Europa.

**1. ROBERT LEWANDOWSKI**

Nyota wa Bayern Munich, Robert Lewandowski yupo kwenye kiwango bora zaidi msimu huu. Mshambuliaji huyo amekuwa aking'ara na miamba hao wa Bavaria tangu kuanza kwa msimu huu.

Raia huyo wa Poland kwa sasa anaongoza katika orodha ya wafumania nyavu katika ligi zote tano za Ulaya, akiwa amefunga mabao 11 katika mechi saba za Bundesliga. Baada ya kuwatungua Tottenham Hotspur kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa sasa amefikisha mabao matatu katika mashindano hayo.

**NAJUA WAJUA**

CHELSEA imetangazwa rasmi kama klabu yenye rekodi mbaya kwa kuwa na idadi kubwa ya kadi za njano kwenye Ligi Kuu England, kutokana na kutokuwapo kwa timu nyingine yenye kadi nyingi kwenye ligi hiyo tangu mwaka 1992.

## SOKA




# UTD LAZIMA IBADILI MBINU 3 KUPATA MATOKEO

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeanza msimu huu wa 2019/20 kwa kusuasua. Kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kipo katika nafasi ya 12 katika msimamo wa Ligi Kuu England (kabla ya mechi za juzi na jana), wakiwa wameshinda mechi mbili tu.

**Mashetani wekundu hao wamepoteza kwa timu kama Newcastle na West Ham, na wameshindwa kufunga mabao, na wameonekana kudumaa katika kila idara.**

Linalohitajika kwa sasa katika kikosi hicho ni kubadilisha mbinu zake ili kuweza kubaki kwenye sita bora, huku wakiwa na changamoto ya kuzipiku timu kama Leicester City na West Ham. Ingawa wana matatizo ya majeruhi, mbinu anazozitumia Solskjaer zinatakiwa kubadilishwa.

Wachezaji wanaonekana kama wamepoteza imani na kocha wao. Hapa tunaangalia mbinu tatu ambazo kocha huyo raia wa Norway lazima azibadilishe ili kuweza 'kuifufua' Manchester United msimu huu:

**1) KUMCHEZESHA GREENWOOD KAMA FOWADI**

Manchester United imekuwa na wakati mgumu wa kupata mabao msimu huu, wakifunga mara tisa tu kwenye Ligi Kuu England. Kuondoka kwa Romelu Lukaku inamaanisha kwamba, United walianza msimu bila kujua nani atakuwa mshambuliaji wa kati, na Anthony Martial na Marcus Rashford wamekuwa na wakati mgumu pale mbele.

Solskjaer anahitaji kumpa nafasi Mason Greenwood kuwa fowadi wa kati. Kinda huyo ana kasi na uwezo mzuri wa kuwa hatari zaidi katika safu ya ushambuliaji ya United.

Muhimu zaidi ni kwamba, kutawafanya Rashford na Martial kurudi kwenye nafasi zao za asili za winga. Huku Rashford na Martial wakiwa kwenye nafasi zao, kutaleta uwiano mzuri katika safu ya ushambuliaji ya Manchester United, kitu ambacho wanakikosa kwa sasa.

Solskjaer hana cha kupoteza kwa kumpa nafasi Greenwood kucheza kwenye fowadi ya kati na Mwingereza huyo anaweza akatengeneza tofauti kubwa katika safu ya ushambuliaji ya United.

**2) MABEKI WA PEMBENI KUSHAMBULIA**

Eneo jingine ambalo United wanashida nalo ni kushindwa kwa mabeki wake wa pembeni kushambulia. Aaron Wan-Bissaka ana uwezo mzuri wa kulinda, lakini mara chache mno anapanda kusaidia mashambulizi.

Pia hilo linaweza kusemwa kwa beki wa kushoto Ashley Young, ingawa mkongwe huyo anacheza tu kwa sababu ya Luke Shaw ni majeruhi.

United inahitaji mabeki wake wa pembeni kusaidia mashambulizi zaidi, kutengeneza pasi za kutoka katika winga zote. Ukichukulia ukweli kwamba, wote Young na Wan-Bissaka ni walinzi wazuri, wana nafasi ya kusukumiza mashambulizi mbele.

Kwa kuweza kwao kupanda mbele wanaweza kupata nafasi ya kuipa wakati mgumu zaidi safu ya ulinzi ya timu pinzani. Hilo litasaidia kutopoteza kwa mipira na washambuliaji wake watakuwa na nafasi nzuri ya kupokea mipira mara kwa mara.

Mabeki wa pembeni kusaidia mashambulizi ni muhimu zaidi katika soka la kisasa, na United wanahitaji kuwatumia zaidi hao.

**3) KUIMARISHA SAFU YA KIUNGO**

United wana wakati mgumu zaidi kwa kiungo wao wanayemtegemea. Paul Pogba amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Nemanja Matic anaonekana ndio anafikia mwisho wake, huku Fred naye amekuwa kwenye kiwango duni na uwepo wa Scott McTominay bado hakujaweza kuisaidia safu ya kiungo.


Wakati Pogba akiwa fiti, Solskjaer anatakiwa kumfanya kuwa ndiye kiungo wa kati wa timu. Kipaji cha Mfaransa huyo kinaweza kuisaidia timu kucheza kwa uhuru huku yeye akiwa anatawala safu ya kiungo wa kati.

Pia hiyo itakuwa sehemu ya McTominay na Andreas Pereira kucheza nyuma yake kama viungo wakabaji.

Mshambuliaji wa Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara, Ditram Nchimbi, ameweka rekodi ya kufunga bao muhimu kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ikiwa ni katika mchezo wake wa kwanza katika kikosi hicho.



NDANI YA 18



BAADA ya kipindi cha usajili, msimu mpya wa ligi za soka za Ulaya umeendelea huku kila klabu ikionyesha na kutumia 'silaha' zake.

Uk. 18



# JUVENTUS WAKIFANYA HIVI VITATU WATASHINDA UEFA

**TURIN,** Italia

MACHO yote yalikuwa kwa Juventus wakati Ligi ya Mabingwa Ulaya ilipoanza msimu uliopita.

**Baada ya kumsajili Cristiano Ronaldo kutoka Real Madrid na kutua pale kwenye dimba la Allianz, kulikuwa na matarajio makubwa mno katika viunga vya Turin kuwa wana nafasi nyingine ya kung'ara kwenye soka la Ulaya.**

Licha ya kuanza msimu huo kwa kutanguliza mguu mbele, ilikuwa bahati mbaya kwamba walishindwa kutimiza ndoto zao. Bianconeri walishinda kuvuka hatua ya robo fainali. Walitupwa nje na vijana wa Ajax ambao walifika nusu fainali.

Kibibi kizee hicho cha Turin bado hakijakata tamaa. Wamerudi msimu huu huku akili yao yote ikiwa kwenye kulitwaa taji hilo. Huku wakiwa na Cristiano Ronaldo kwenye timu yao, kwa uhakika wanajiona kwamba wana nafasi ya kulibeba taji hilo.

Hata hivyo, wanahitaji vitu hivi vitatu kuweza kutimiza ndoto yao hiyo kama makala hii inavyochambua:

### 3. KUIMARISHA KIWANGO CHA RONALDO

Cristiano Ronaldo alikuwa mtu mwenye ushawishi zaidi pale Juventus ili kuweza kulibeba taji hilo msimu uliopita kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia zaidi. Bado pamoja na kiwango chake, Bianconeri walishindwa kutimiza ndoto zao kupitia kwa Mreno huyo.

Ronaldo alimaliza michuano hiyo akiwa na mabao sita tu kwa jina lake katika mechi tisa alizocheza. Hata hivyo, hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kwake kushindwa kuwa kwenye ubora zaidi katika mashindano hayo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Wakati wa msimu wa 2017/2018, Ronaldo alifunga mabao 15 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa pale Real Madrid. Alimaliza akiwa na mabao 12 katika msimu wa 2016/2017, huku msimu wa 2015/2016 pia alifunga mabao 16. Ukilinganisha hilo na msimu uliopita, ni wazi kwamba Juve hawakuweza kupata huduma yake bora.

Hivyo, timu yake inahitaji kuimarisha zaidi safu ya ushambuliaji msimu huu ili kuweza kumpa sapoti nzuri zaidi Ronaldo. Kiwango chake bado kina nafasi ya kuiwezesha Juve kulibeba taji hilo.

### 2. PLANI B KWA RONALDO

Ronaldo alithibitisha msimu uliopita kwamba yeye ni mtu wa kwenye matukio makubwa na mwenye kuwa na uwezo wa kuamua matokeo wakati wa hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alikuwa nyota wa mchezo dhidi ya Atletico Madrid pale Turin na itakuwa moja ya kumbukumbu bora zaidi katika maisha yake ya soka.

Licha ya kuonyesha kiwango chake, lakini Juventus walionyesha kwamba walikuwa wakimtegemea yeye tu. Bianconeri walishindwa kufanya lolote bila Ronaldo. Mreno huyo alionekana kuwa ndiye aliyeibeba timu.

Ukweli ni kwamba alifunga mabao yote ya Juve katika hatua ya mtoano na timu ilimtegemea yeye tu. Ingawa Ronaldo ana uwezo mkubwa wa kuamua matokeo kwenye mchezo wowote, kuwa na mpango B wa Ronaldo kutawasaidia Bianconeri hao kupata matokeo bora zaidi

.

### 1. KUWAPA NAFASI WACHEZAJI VIJANA


Juve msimu uliopita kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ilibebwa zaidi na wachezaji wakongwe. Ingawa uzoefu ni suala la msingi kwenye mashindano hayo, imethibitisha mara kadhaa kwamba wachezaji wakongwe wanapata tabu sana wakikutana na timu zenye vijana tupu. Na hilo lilitokea dhidi ya Ajax.

Bianconeri hao walishindwa kabisa kutamba mbele ya vijana Ajax wakati walipotolewa katika hatua ya robo fainali. Walishindwa kuhimili vishindo vya vijana hao kutoka kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie. Walionekana kuchoka mapema na wakajikuta wakitupwa nje ya mashindano hayo, licha ya Ronaldo kujaribu kuwabeba.

Msimu huu Bianconeri hao wanahitaji kuwatumia zaidi vijana ili waweze kutamba. Matthijs De Ligt alisajiliwa kipindi cha majira ya joto. Beki huyo anatakiwa kupewa nafasi ya kuonyesha ubora wake kwenye timu. Wachezaji wengine vijana kama Rodrigo Bentancur na Merih Demiral pia wanahitaji kupewa nafasi zaidi.

Wachezaji hawa vijana wanatakiwa kupewa nafasi zaidi ya kucheza na kuthibitisha ubora wao.

**USILOLIJUA**



KLABU ya Barcelona ambayo ilikuwa inataka kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Robert Firmino, imefuta mpango huo na sasa inajipanga kumnasa Marcus Rashford kutoka Manchester United ili kumrithi Luis Suarez.



# Huduma wagonjwa wa dharura kwa gari zaanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya imeanza kutoa huduma ya magonjwa ya dharura kwa kutumia gari yenye vifaa vya matibabu ambalo husafirisha wagonjwa kutoka eneo alilopo hadi hospitalini huku akiendelea kupata matibabu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwaji, wakati wa bonanza la kuazimisha miaka 34 ya kuanzishwa kwa hospitali hiyo kwenye viwanja vya Chuo cha Uhasibu (TIA) Tawi la Mbeya na kuhususisha shughuli mbalimbali ikiwamo michezo na kupima afya.

Dk. Mbwanji alisema huduma ya magonjwa ya dharura kwa kutumia gari yenye vifaa vya matibabu ilianza tangu Agosti mosi mwaka huu na kwamba gari hilo hufika kila eneo ambalo mgonjwa hutoa taarifa.

Alisema lengo la kutoa huduma hiyo ni kupunguza vifo kwa wagonjwa wa dharura ikiwamo wenye matatizo ya presha, ajali na moto na kwamba huchangia gharama ndogo ya usafiri kulingana na eneo alilopo na kupata huduma akiwa ndani ya gari.

"Tunajivunia hospitali yetu kuwa na huduma ya ambulance kwa wagonjwa wa dharura tunapopigiwa simu kwa sababu tumetoa namba za simu na mgonjwa analazimika kuchangia gharama za usafiri kulingana na eneo analotoka, gari yetu ina vifaa vyote vya matibabu pamoja na wataalamu wa afya ambao huhudumia mgonjwa alisema," Dk. Mbwanji.

Mgeni rasmi katika bonanza hilo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipongeza hatua ya hospitali hiyo kuanzisha huduma hiyo, na kwamba itasaidia kuokoa uhai wa wagonjwa kwa haraka.

Alisema huduma hiyo ni rafiki kwa wagonjwa kwani inawafikia kwa haraka aliwataka wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutumia huduma hiyo.

Daktari anayeshughulikia magonjwa ya dharura katika hospitali hiyo, Dk. Prosper Bashaka, alisema katika kipindi cha mwaka 2018 walipokea jumla ya wagonjwa 4,500 huku asilimia 25 wakiwa ni wa ajali za barabarani.

Dk. Prosper alisema asilimia 25 ya wagonjwa wanatokana na ajali za barabarani ambazo chanzo chake magari ya mizigo, abiria, bajaji na pikipiki.

Aliongeza kuwa tangu Januari mwaka huu hadi Oktoba takribani wagonjwa wa dharura 35000 walifikishwa hospitalini hapo, na kwamba idadi hiyo ni kubwa.

Muuguzi kitengo cha wagonjwa wa dharura, Rose Mpayo, alisema tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo wamehudumia wagonjwa wanne ambapo kati yao watatu walitokea Halmashauri ya Jiji la Mbeya na mmoja akitokea Mji wa Vwawa wilayani Mbozi.

Alisema mwitikio bado ni mdogo kwa wagonjwa aliwahamasisha kutumia huduma hiyo kwa sababu inaokoa uhai wa mtu kwa muda mfupi kabla ya kufika kwenye hospitali na kwamba mgonjwa anao uhuru kwa kuchagua na kupelekwa hospitali yeyote aitakayo nchini wakati anaendelea kupatiwa huduma.



Daktari anayeshughulikia magonjwa ya dharura katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Prosper Bashaka, akitoa ufafanuzi wa namna gari lenye vifaa vya matibabu (Ambulance) linavyoweza kutoa huduma za matibabu kwa majeruhi na wagonjwa wengine wakiwamo wa presha wanaweza kutibiwa ndani ya gari hilo, kabla ya kufika hospitalini lengo likiwa ni kuokoa maisha ya wagonjwa kwa haraka zaidi, wakati wa bonanza la kusherehekea miaka 34 tangu kuanzishwa kwa hospitali hiyo. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Sheria ya kubana uvamizi mifugo mashambani yaja

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imesema ipo kwenye mchakato wa kutunga sheria ndogo ya ulipaji faini kwa wafugaji wanaoruhusu mifugo yao kuvamia mashamba ya wakulima ili kumaliza kabisa changamoto ya migogoro wilayani humo.

Hayo yalisemwa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Halmshauri ya Wilaya ya Mbarali, Aswege Kaminyoge, wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani.

Alisema wamefikia hatua ya kuanza mchakato wa kutunga sheria ndogo itakayowabana wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye mazao baada ya sheria mama iliyopo kutokuwa na makali ya kuzuia wafugaji hao.

Alisema sheria iliyopo inatoa adhabu ndogo kwa wafugaji kulipa fidia au faini pindi wanapokamatwa wakiingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kwa sababu wanao uwezo wa kulipa, hivyo sheria mpya ikikamilika itaongeza uzito wa adhabu.

"Wilaya yetu imekuwa na migogoro ya mara kwa mara kati ya wafugaji na wakulima hali hiyo inasababishwa wafugaji kutoogopa kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kwa sababu wanao uwezo wa kulipa faini sasa tukifanikiwa kutunga sheria hiyo tutaweza masharti magumu ili kukomesha vitendo hivyo," alisema Kaminyoge.

Aliongeza kuwa ili kupatikana kwa sheria hiyo ndogo ya kudhibiti wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima, wanaanda waraka kupeleka Wizara ya Ardhi ili itoe mwongozo wa namna ya kukamilisha mchakato huo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Brown Mwakibete, alisema kuwapo kwa sheria mpya ya kudhibiti wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kutasaidia kuepukana na mapigano ambayo yamekuwa yakigharimu maisha ya watu.

Aliongeza kuwa uwapo wa sheria hiyo utasaidia kupunguza mapigano baina ya wakulima na wafugaji ndani ya wilayani hiyo ili kila mmoja kwa nafasi yake aweze kufanya kazi zake za uzalishaji wa amani.

# NSSF yakuna wajasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAJASIRIAMALI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wamepongeza hatua ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuanzisha mfuko wa mafao kwa sekta zisizorasmi kwa madai itasaidia kutimiza malengo yao.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wajasiriamali wa kutengeneza batiki na sabuni kutoka Kata ya Ijombe, Flora Mlowezi wakati wa kilele cha maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali yaliyofanyika katika viwanja vya stendi ya mabasi iliyopo Mji wa Mbalizi. Mlowezi alisema NSSF imefanya jambo jema kuzikumbuka sekta zisizo rasmi kuziweka katika hifadhi hiyo kwani itawasaidia kujilimbikizia mafao yao kupitia shughuli wanazozifanya ikiwamo ujasiriamali na kilimo.

"Tumefurahi hatua ya NSSF kuanzisha mafao kwa sekta zisizorasmi hakika itatusaidia kuwekeza fedha nyingi ambazo zitasaidia kufanya shughuli za maendeleo kwa baaadae ikiwamo kusomesha watoto na ujenzi," alisema Mlowezi.

Felix Benard, anayejihusisha na usindikaji wa asali kutoka Kata ya Ihango, alisema maonyesho hayo yamemsaidia kujifunza mbinu za kuongeza thamani wa bidhaa na ushauri wa kitaalamu kupitia Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema atahakikisha anazalisha asali kwa wingi na kiwango cha ubora zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa awali ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Mbeya, Nurdin Mruma, alisema lengo la kuanzisha mfuko wa mafao kwa sekta zisizo rasmi ni kuhakikisha wajasiriamali, wakulima na madereva bodaboda au bajaji kupata fedha za kijikimu anapofikia umri wa kuzeeka au kushindwa kufanya kazi. Alisema moja ya faida ya mafao hayo kwa sekta isiyo rasmi ni kwamba mkulima au mjasirimali anatakiwa kulipa fedha kuanzia kiasi cha Sh. 20,000 kila mwezi na kwa mkulima atalipa kulingana na msimu wa mavuno lakini usipite mwaka mzima.

Aliongeza kuwa hakuna masharti magumu yanayomzuia mtu kuchukua mafao yake muda wowote anaposhindwa kuendelea kulipa ukilinganisha na walio kwenye sekta rasmi.

Mwitikio umekuwa mkubwa sana ya watu wasio kwenye sekta rasmi kujisajili na mfuko huu wa mafao ambao unawawezesha kujilimbikizia mafao yao ili iwasaidie watakapokuwa wazee au kuchoka kuendelea na shughuli za uzalishaji, nawashauri na wengine kujiunga kwa sababu hakuna masharti magumu alisema Mruma.

Maonyesho wa shughuli ya wajasiriamali wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, yaliratibiwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la CRS kwa kushirikiana na wadau wengine.





# Vijana wasuasua mikopo

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

IMEELEZWA kumekuwapo na mwitikio mdogo kwa vijana kuomba mikopo inayotolewa na halmashauri na kusuasua kwenye urejeshaji wake ikilinganishwa na wanawake.

Mwaka 2018, serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ambapo pamoja na mambo mengine, iliweka kisheria halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Kauli hiyo ilitolewa na Mratibu wa Maendeleo ya Vijana na Watoto wilayani Chamwino, Sophia Swai, kwenye uzinduzi wa mradi wa kuwawezesha vijana kukamata fursa za kiuchumi wilayani humo unaofadhiliwa na Shirika la Civil Foundation.

Alisema kumekuwapo na vijana wachache sana wanaoomba mikopo iliyotengwa kwa ajili yao na kwamba hata wakipewa urejeshaji wao si mzuri tofauti na wanawake.

Alitolea mfano katika mwaka wa fedha 2018/19 Halmashauri ya Chamwino ilitoa Sh. milioni 105.1 kwa vikundi 33 kati ya hivyo vikundi vya vijana ni nane.

"Sababu ni vijana kutaka matokeo ya haraka, tumechukua hatua kwa kuagiza maofisa watendaji kulifanya suala kuwa ajenda ya kudumu katika mikutano yote ili wahamasike kukopa," alisema.

Pia alisema kupitia mradi wa Shirika linaloshughulika na Kuhamasisha Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira (Donet) ambao wameanzisha mradi wa kuwawezesha vijana kukamata fursa za kiuchumi wilayani humo, utasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mratibu wa mradi huo kutoka Civil Foundation, Emmanuel James, alisema vijana wa vijiji sita wilaya ya Chamwino watanufaika na mafunzo kwa vijana juu ya kukamata fursa.

"Maeneo mengi hasa vijijini vijana wanakuwa na shughuli moja ya kilimo, lakini baada ya hapo wanakuwa na likizo ndefu sasa mradi huu wa miezi minane unalenga kuhamasisha vijana kuwa na shughuli za kila siku ambazo zitawaongezea kipato na kujiinua kiuchumi," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Agnes Mweso, aliwaasa vijana kuthubutu kufanya shughuli itakayowafanya kuinua vipato vyao kwa kuchangamkia fursa kwenye maeneo yao.

# Klabu 776 za kupinga rushwa zafunguliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KLABU 776 za kupinga rushwa zimefunguliwa mkoani Dodoma na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ili kutoa elimu na kutokomeza rushwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema klabu hizo zimeundwa kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kuzuia, kupokea au kutoa rushwa.

"Tumefungua jumla ya klabu 776,katika shule za msingi, sekondari na vyuo, kwa shule ya msingi tumefungua klabu 545 ambapo ni sawa na (72%), sekondari 209 (93%); na vyuo 22 (79%),"alisema.

Aidha, alisema bado shule za msingi 209, sekondari 15 na vyuo sita ili waweze kufikia asilimia 100.

Alieleza kuwa zikikamilika kufunguliwa kwenye maeneo hayo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuelimisha jamii.

"Lengo letu ni kuona kila eneo kuna klabu ambazo ziko imara na zinasaidia kuwaelimisha jamii hususan maeneo ya vijijini ambapo wengi wao walikuwa hawana uelewa juu ya madhara ya rushwa," alisema. Alisema hadi sasa wamefanikiwa kwa asilimia 76 ya kuanzisha klabu hizo, na kuwataka wananchi kuendelea kuzingatia umuhimu wa elimu inayotolewa.

Hata hivyo, aliwashauri wananchi kutumia haki zao za msingi kuchagua viongozi waadilifu watakaoiongoza mitaa na vijiji ili kuleta maendeleo ya wananchi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Kibwengo alisema Takukuru wanaamini kila mwananchi akitumia haki yake ya msingi atafanikiwa kuchagua viongozi bora ambao watasimamia kwa weledi miradi inayotekelezwa na serikali.

"Nawasihi wananchi chagueni viongozi bora na wala msikubali kurubuniwa na rushwa ndogo ndogo ambazo hazitowasaidia chochote," alisema Kibwengo.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali, Vicky Bishubo, wakati alipotembelea banda la Benki ya NMB katika uzinduzi wa Maonyesho ya Viwanda na Biashara na kongamano kubwa la uwekezaji Mkoa wa Pwani jana. **PICHA; MPIGAPICHA WETU**

# Walimu kupokwa mashamba ya shule

**Na Mwandishi wetu,** KONGWA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, ameagiza mashamba yote ya shule za msingi na sekondari yaliyokuwa yakitumiwa na walimu kurejeshwa ili yatumike na shule husika kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula.

Dk. Nkullo alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki kufuatia maazimio ya kamati lishe wilayani humo yaliyotolewa kwenye kikao cha kujadili taarifa za lishe.

Alisema mashamba hayo yakirejeshwa yatatumiwa na wanafunzi kulima mazao ambayo yatawapatia chakula na kuboresha lishe yao.

Dk. Nkullo ambaye ni mwenyekiti wa kamati hiyo, alisema jukumu la kamati hiyo ni kujenga jamii yenye kuzingatia lishe bora nyumbani na shuleni.

"Kamati iliazimia kuwa, shule za msingi na sekondari Kongwa kurudisha elimu ya kujitemea na kuhakikisha mashamba yote ya shule yaliyokuwa yanalimwa na walimu yalimwe na shule," alisema.

Alibainisha kwa shule zote zisizo na mashamba zitafutiwe pamoja na kuanzisha bustani za mboga na matunda pamoja na uvunaji wa maji na mvua ili kusaidia umwagiliaji kipindi cha kiangazi.

"Pia tumeazimia ufanyike utafiti wa masuala ya lishe mwaka huu ili kujua takwimu halisi za hali ya lishe iliyopo sasa, tumewashirikisha wadau wa lishe ikiwamo Shirika la Save the Children, CUAMM na Ufundiko ili nao waangalie namna ya kusaidia utafiti huo utakaogharimu Sh. milioni 22," alisema.

Naye Katibu wa Lishe ambaye ni Mganga Mkuu wa Hospitali ya Kongwa, Dk. Thomas Samuel, alisema wamejipanga kuhakikisha wanatatua changamoto ya upungufu wa vifaa vya kupimia hali ya lishe kwenye vituo vya afya na zahanati ikiwamo kuchora ukutani ubao wa kupimia urefu kwa kufuata vipimo vya kitaalamu.

Ofisa Kilimo wa wilaya hiyo, Jackson Shija, alisema takribani wakulima 1,233 wa kata za Kongwa, Ngh'umbi na Ugogoni wa vijiji 12 wamepata mafunzo ya namna bora ya uhifadhi wa mazao kwa kutumia teknolojia za Hermatics Bags na Vihenge vya Chuma.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya chakula na kupunguza upikaji wa pombe za nafaka.

Kadhalika, alisema kutokana na uwepo wa Kampeni ya Ondoa Njaa Kongwa (ONJAKO) ambayo inahimiza kilimo cha zao la mtama kwa miaka 3 mfululizo hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuimarika.





Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, Zanzibar, Simai Mohamed Said (kushoto), akishiriki ujenzi wa nyumba ya Mzee Khalfan Mhoja (76) mkazi wa Kiongoni Zanzibar jana, aliyeangukiwa na nyumba yake hivi karibuni kutokana na mvua zinazoendelea. Kulia ni Diwani mstaafu wa Wadi ya Tunguu, Shabani Jabu na mtoto wa Mwakilishi huyo, Ayana Said Simai. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mama Mwanamwema awafunda wajasiriamali

**NA Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mwanamwema Shein amesema shughuli za ujasiriamali zinahitaji taaluma ili kuondoa changamoto na kufanyika kwa ufanisi na kuleta tija.

Mama Mwanamwema alisema hayo katika ufunguzi wa kongamano la wajasiriamali wanawake wa mikoa ya Unguja, hafla iliyofanyika Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja. Alisema shughuli za ujasiriamali kama ilivyo nyingine zinahitaji elimu ya nadharia na vitendo ili kumwezesha mjasiriamali kupata tija na kuongeza kipato katika familia.

Alisema kwa kuelewa umuhimu wa shughuli za ujasiriamali kwa wananchi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeunda Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, pamoja na kaunzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili kufanikisha azma hiyo.

Mama Mwanamwema alieleza kuwa serikali imeandaa mipango mbalimbali ya kuwasaidia wananchi ili kuongeza kipato na kuwataka wananchi kuzitumia ipasavyo fursa zilizopo ili kuongeza kipato cha familia.

Vile vile, alipongeza Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT), kwa uamuzi wa kuandaa kongamano hilo, ambalo pamoja na mambo mengine linazungumzia umuhimu wa kuimarisha daftari la wapigakura.

Alisema wakati huu wanachama wa CCM wakijiandaa kushiriki uchaguzi mkuu ujao mwakani, kuna umuhimu wa kukumbushana umuhimu wa kuimarisha daftari la kudumu la wapigakura na kutoa wito kila mmoja kushiriki na kutekeleza wajibu wake wakati utakapofika.

"Tusisahau kuwa sisi kinamama na vijana ndio tulio wengi na tegemeo la chama chetu kukipatia ushindi wa kishindo, nasaha zangu nyote utakapofika wakati mtekeleze wajibu wenu," alisema. Aliwapongeza wajasiriamali walioshiriki kwenye kongamano hilo, kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kufanikisha azma yake ya kuinua kipato na hali za wananchi wake.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, alimpongeza mama Mwanamwema kwa mchango mkubwa anaoutoa kusaidia harakati za ujasiriamali kwa kinamama.

Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Thuwayba Edington Kisasi, alisema ni lengo la jumuiya hiyo kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu ya ujasiriamali nchi nzima. Aliwataka washiriki wa kongamano hilo kuitafutia ufumbuzi changamoto ya udhalilishaji wa kijinsia, akibainisha chanzo chake kinatokana na jamii kuondokana na utamaduni, mila na silka za Wazanzibari.

## Aeleza umuhimu ushirikishaji wadau kwenye majanga

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

NAIBU Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Muhidini Ali Muhidini, amesema mawazo ya pamoja yanahitajika kuipitia rasimu ya mkataba wa utoaji huduma kwa mteja ili kuimarisha huduma bora.

Alieleza hayo wakati wa kikao cha kuipitia rasimu ya mkataba wa utoaji wa huduma kwa mteja ambao ulishirikisha washiriki kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema ipo haja ya kuimarisha mkataba wa utoaji huduma kwa mteja ili kutoa huduma bora zikazosaidia kukuza kiwango cha uwelewa kwa wateja pale wanapofikwa na majanga.

Alisema jamii imekuwa ikikumbwa na maafa mbalimbali kulingana na vipindi husika kama wakati wa mvua au magonjwa ya mlipuko hivyo rasimu hiyo inapaswa kutolewa michango ambayo itaisaidia jamii pale inapokumbwa na maafa au majanga hapa nchini.

Mkuu wa kitengo cha mipango utawala na rasilimali watu, Haji Faki Hamdan, akizungumzia huduma wanazitoa kupitia kamisheni hiyo ya kukabiliana na maafa, alisema ni pamoja na kusimamia shughuli zote za misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa maafa nchini.

Washiriki wa kikao hicho walitoa michango mbalimbali ya kuimarisha rasimu hiyo ya mkataba wa utoaji huduma kwa mteja.

# Serikali yaahidi kuendeleza Sekta ya Elimu

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Wizara ya Habari Utalii na Mambo ya Kale, Choum Kombo Khamis, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendeleza jitihada za kuimarisha sekta ya elimu ili taifa liweze kupata vijana wenye taaluma katika fani tofauti licha ya kuwapo changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo. Aliyasema hayo katika hafla ya kuwapa vyeti wanafunzi wa awamu ya pili walioomaliza mafunzo kutoka Shirika la Internews kupitia mradi wa boresha habari katika Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar, Kilimani. Khamis alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha kiwango cha elimu kinachotolewa na vyuo vya Zanzibar ikiwamo chuo cha habari kinakwenda sambamba na matakwa ya soko la ajira pamoja na mahitaji mengine ya kijamii kwa maendeleo ya taifa.

Akizungumzia mafunzo hayo, alisema hatua hiyo ya mafunzo waliopata ni muhimu ambayo yatasaidia kuhamasisha uwajibikaji na hata waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa weledi ikiwamo kuzingatia maadili yao na kuandika habari zinazoibua mambo mbalimbali kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi au kuelimisha jamii. Mkuu wa Chuo hicho, Aiman Duwe, aliwataka wanafunzi hao kuyafanyia kazi mafunzo waliyoyapata kutoka Internews ili waweze kuleta ufanisi zaidi katika ufanyaji kazi zao.

Hata hivyo, aliwataka kutotosheka na elimu waliokuwa nayo bali wajiendeleze ili waweze kusonga mbele katika elimu zao ikilinganishwa na soko la ajira lilipo hivi sasa linategemea zaidi wasomi.

# Waziri aagiza hatua sakata kontena 38 chuma chakavu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais imepokea ripoti ya uchunguzi wa kontena 38 za chuma chakavu zilizokuwa zisafirishwe nje.

Hata hivyo, kontena hizo ziliizuiliwa bandarini Dar es Salaam.

Ripoti imeeleza kuwapo kwa udanganyifu mkubwa wa kusafirisha bidhaa ambazo hazimo katika orodha ya vitu vilivyoruhusiwa kusafirishwa nje kama chuma chakavu au taka hatarishi.

Akipokea taarifa hiyo, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, alisema uchunguzi umeibua mambo mengi na kwamba serikali itawachukulia hatua kali wahusika wote katika kashfa hiyo.

"Ripoti inaonyesha kumekuwapo kwa hujuma kubwa ya miundombinu ya nchi; kwa mfano mifuniko ya chemba za maji, nyaya za umeme, mataluma ya reli kinyume cha sheria na taratibu za biashara ya chuma chakavu," alisema na kuongeza:

"Ripoti imebaini hata kuwapo kwa kampuni isiyo na kibali cha kufanya biashara hiyo. Tutaifutia leseni ya biashara kampuni hiyo na nyingine zitakazoonekana zimefanya udanganyifu na kuhujumu uchumi wa taifa."

Simbachawene alifanya ziara katika Bandari ya Dar es Salaam Agosti 9, mwaka huu. Baada ya kuyaona makontena 38 ya chuma chakavu yaliyozuiliwa bandarini, aliliagiza Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamzi wa Mazingira(NEMC) kuwasilisha serikalini taarifa juu ya makontena hayo. Alieleza kuwa katazo la serikali la kusafirishwa vyuma chakavu na taka hatarishi nje ya nchi limetokana na udanganyifu mkubwa wa wafanyabiashara. "Katazo hilo lengo lake ni kulinda viwanda vyetu vinavyotegemea vyuma chakavu kama malighafi ya kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo nyaya za umeme na mikeka ya plastiki."

Simbachawene alisema ni muhimu kulinda viwanda vilivyopo nchini kwa kuzuia malighafi kama chuma chakavu kusafirishwa nje ya nchi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na pia kuzalisha ajira nchini. "Ameeleza kuwa azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda itafanikiwa iwapo kuna malighafi kwa ajili ya viwanda vya ndani. Aidha, ametangaza kwamba kuanzia sasa hatoruhusiwa mtu yeyote kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ama kupeleka kiwandani kwa ajili ya kurejeleza mali bila kibali kutoka kwa waziri na kwamba mamlaka za serikali za mitaa ndizo zitakazosimamia ukusanyaji wa vyuma chakavu na taka hatarishi kwa ngazi ya mtu mmoja mmoja.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alieleza kuwa licha ya sheria kumtaka mfanyabiashara wa chuma chakavu kujaza fomu namba tatu inayoonyesha anakopata mali hiyo hakuna mfanyabiashara aliyefanya hivyo.




Mkuu wa Kanda ya Mashariki wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi Lawi Odiero, akikabidhi kitabu cha mwongozo wa mawasiliano kwa mwananchi aliyetembelea maonyesho ya Wiki ya Viwanda Mkoa wa Pwani, yanayofanyika katika Viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wameonywa upotoshaji chanjo dhidi watoto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imeonya baadhi ya wazazi kupotosha utolewaji wa chanjo ya surua, rubella pamoja na polio, ambayo inatolewa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Lengo ni kuwakinga kupatwa na magonjwa mbalimbali, pamoja na kutokomeza vifo vya watoto wadogo.

Angalizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, kwenye uzinduzi wa chanjo ya hiyo uliofanyika kwenye Kata ya Lyabukande Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, kuwa wazazi wajitokeze kwa wingi kupeleka watoto wao kupatiwa chanjo ambayo itawakinga na magonjwa.

Alisema kumekuwapo na tabia kwa baadhi ya wazazi kupotosha kuhusu chanjo kwa watoto wadogo, kuwa zinawasababishia kupatwa na maradhi mengine, hivyo kusababisha utolewaji wake kusuasua.

"Naonya wazazi ambao mtapotosha chanjo ya surua, rubella na polio, kwa atakayebainika kufanya hivyo, serikali haitasita kumchukulia hatua kali," alisema Telack.

"Chanjo hizi zinatolewa bure ambapo serikali yenu imegharamikia, hivyo hakuna mzazi yeyote kutoa pesa, na ambaye ataombwa pesa atoe taarifa ili mhusika tupate kumshughulikia," aliongeza.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashidi Mfaume, alifafanua kuwa watoto ambao watapatiwa chanjo hiyo ni 286,124, polio ni 151,547. Utoaji huo wa chanjo ulianza jana hadi 21, mwaka huu.

Mmoja wa wazazi ambao walipeleka watoto wao kupatiwa chanjo hizo, Monica Shija, alikiri kuwapo na upotoshaji wa utolewaji wa chanjo hizo, lakini baada ya kupatiwa elimu wakaona ni uongo, hivyo kuhamasika kupeleka watoto wao kupewa chanjo ili kuwakinga dhidi ya magonjwa.

# Wadau waujadili mpango blue print

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka wadau wa sekta binafsi kuhakikisha wanarasimisha biashara zao ili waweze kupata matokeo chanya yanayofanywa katika muongozo wa uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Rai hiyo imetolewa mkoani Morogoro na Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti wa Ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Gervas Kaisi, wakati wa Mkutano ulioandaliwa na Baraza la kilimo Tanzania kwa kushirikiana na programu ya kuimarisha mifumo ya masoko katika Mnyororo wa thamani (AMDT). "Tangu tumezindua Blue Print ni kweli Serikali imefanya maboresho makubwa hasa kwenye tozo ambazo zilikuwa ni kero kwa wafanyabiashara, lengo kuu ni kuhakikisha tunaboresha mazingira ya ufanyaji biashara, kwa sasa zaidi ya tozo 150 tumekwisha kuzitoa,

"Lakini pia hatua nyingi zinachukuliwa na Taasisi mbalimbali za Serikali za kuunganisha mifumo yake kwenye mtandao ili iwe rahisi katika upatikanaji wa huduma na tayari kuna taasisi zimekwisha kutekeleza suala hilo," alisema.

Wadau hao wa sekta binafsi wametakiwa kuhakikisha wanaendelea kutoa maoni yao kuhusu muongozo huo ambao utekelezaji wake umaeanza mapema mwaka huu 2019 na kwamba ni muhimu mapendekezo hayo yakaendana na nini wangepata seriklai ifanye.

"Kama ukisema tozo ni muhimu useme aina ya tozo inayokukera ili tuweze kuifanyia kazi kikamilifu, lakini pia ni muhimu sana hata kama kuna kanuni inakukera katika biashara zako tuambie kwa kuitaja kabisa aina ya kanuni hiyo na serikali ni sikivu tutatekeleza," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya Baraza la Kilimo Tanzania, Omary Mwaimu, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano huo wa siku moja uliowajumuisha wadau kutoka Sekta binafsi na maafisa kadhaa kutoka Serikalini amesisitiza wadau wa Sekta binafsi hasa katika Sekta ya Kilimo kurasimisha biashara zao. Mtaalamu Mwelekezi na Utetezi kutoka AMDT, Tertula Swai, alisema Mkutano huo ni muhimu kwani lengo lake kuu ni kuwajengea uwezo Sekta binafsi kufanya majadiriano na Serikali kuhusu vipaumbele vilivyomo ndani ya Muongoz huo na kwamba AMDT iko kwa ajili ya kuimarisha Baraza la Kilimo pamoja na maboresho katika maeneo ya serikali yanayohitaji kuboreshwa.

## HABARI KIMATAIFA

# Wavalishwa maboksi wakifanya mtihani

**HAVERI,** India

MAOFISA katika shule moja nchini India wameomba msamaha baada ya picha ya kushangaza ya wanafunzi waliovalia maboksi vichwani wakifanya mtihani kusambaa katika mitandao ya kijamii.

Picha hizo zilipigwa wakati wa mtihani wa kemia katika Shule ya Upili ya Bhagat mjini Haveri, Jimbo la Karnataka.

Picha hizo ziliwaonyesha wanafunzi wakiwa wamevalia maboksi yaliokatwa upande mmoja, ili kuwazuia wasiibie kazi ya wenzao.

**Nilipopata ujumbe kuhusu kisa hicho, nilitoa agizo kwa usimamizi wa shule kusitisha mpango huo mara moja.**

Msimamizi wa shule hiyo ameomba radhi kwa maofisa wa wilaya wa elimu kufuatia kisa hicho.

MB Satish aliliambia Shirika la utangazaji la BBC kuwa waliamua kutumia mbinu hiyo isiokuwa ya kawaida kukabiliana na visa vya udanganyifu wakati wa mtihani.

Alisema kuwa shule hiyo ilichukua hatua hiyo kama sehemu ya majaribio baada ya kusikia inatumika katika maeneo mengine nchini.

Pia alisisitiza kuwa wanafunzi wenyewe waliridhia kuvalia maboksi hayo vichwani wakati wa mtihani na kuongeza kuwa walikuja nayo wenyewe.

"Hakuna mwanafunzi aliyelazimishwa kuvalia boksi kichwani. Kama unavyoona katika picha hizi kuna baadhi ya wanafunzi ambao hawakuvaa, waliokuwa wamevalia pia baadhi yao walivua baada ya dakika 15, wengine baada ya dakika 20 na hata sisi wenyewe tuliwaambia wayavue baada ya saa moja," alisema Peerjade ambaye ni Naibu Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi ya shule hiyo.

Maofisa wa elimu wa kikanda waliripotiwa kufika shuleni hapo kulalamikia hatua hiyo muda mfupi baada ya picha hizo kusambazwa katika mitandao ya kijamii.

"Nilipopata ujumbe kuhusu kisa hicho, nilitoa agizo kwa usimamizi wa shule kusitisha mpango huo mara moja," alisema Peerjade aliponukuliwa na gazeti la Time nchini India.

Wakuu wa shule hiyo walieleza kuwa wamekomesha zoezi hilo kufuatia maagizo kutoka kwa bodi ya shule. **BBC**



Wanafunzi wakiwa wamevaa maboksi kichwani kwenye chumba cha mtihani nchini India. **PICHA: BBC**

# Uingereza yatuma barua 3 EU kisa Brexit

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson ametuma barua tatu kwa Umoja wa Ulaya (EU).

Johnson alituma barua hizo juzi jioni baada ya Bunge la Uingereza kupiga kura ya kuchelewesha kuufanyia uamuzi mpango wake wa Brexit.

Barua ya kwanza kutoka kwa Waziri Mkuu Johnson ilitumwa kwa Rais wa Baraza la Ulaya, Donald Tusk. Barua hiyo ambayo haikutiwa saini na Waziri Mkuu Johnson ni nakala ya rasimu iliyomo katika sheria za Uingereza inayomlazimu Waziri Mkuu kuomba kurefushwa muda wa mchakato wa Brexit.

Barua ya pili iliyopelekwa kwa EU ni kuhusu pingamizi la Waziri Mkuu huyo wa Uingereza dhidi ya kurefushwa muda wa Brexit.

Wziri Mkuu Johnson alisema kurefushwa muda wa mazungumzo ya mchakato wa Brexit litakuwa ni kosa kubwa. Barua ya tatu ilitoka kwa Balozi wa Uingereza katika Umoja wa Ulaya, Tim Barrow na kupelekwa kwa Jumuiya kwa niaba ya Waziri Mkuu Boris Johnson.

Ujumbe wa Waziri Mkuu wa Johnson uliomo kwenye barua hiyo iliyochapishwa kwenye mtandao wa Twitter na mwandishi mmoja wa gazeti la Financial Times mjini Brussels unasema.

"Nimeweka wazi tangu nilipochukuwa madaraka ya uwaziri mkuu na nimerudia hayo kwa wabunge siku ya Jumamosi kwamba maoni yangu, na msimamo wa serikali yangu, kuhusu kuongeza zaidi wa mchakato wa Brexit kutaharibu masilahi ya Uingereza na ya washirika wetu wa Umoja wa Ulaya na kwamba hatua hiyo itavuruga uhusiano kati yetu," ilieleza barua hiyo.

Rais wa Halmashauri ya Ulaya, Donald Tusk alithibitisha kupokea barua ya maombi ya kurefushwa mchakato wa Brexit na alisema ataanza kujadili suala hilo na viongozi wa EU.

Wakati huo huo, maelfu ya watu waliandamana mjini London siku ya Jumamosi wakitaka kura nyingine ya maoni kuhusu nchi hiyo kujitoa kwenye EU.

Waandamanaji hao walisherehekea pia hatua ya bunge la nchi hiyo kupiga kura ya kuahirisha kwa muda mchakato wa Brexit. Wengi wa waandamanaji hao walisafiri umbali mrefu kutoka maeneo mbalimbali ya Uingereza hadi jijini London kushiriki kwenye maandamano hayo. **DW**

## Kiongozi upinzani akutana na Rais Salva Kiir

**JUBA,** Sudan Kusini

KIONGOZI wa upinzani Sudan Kusini, Riek Machar amerudi nchini humo siku ya Jumamosi na kukutana na Rais Salva Kiir ikiwa umebakia muda mfupi kabla siku iliyopangwa kwa viongozi hao kuunda serikali ya umoja wa kitaifa, kumaliza vita.

Katika ziara yake hiyo ya siku mbili, Machar anatarajiwa kukutana na Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, ambaye atawasili na ujumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Ujumbe huo unatarajiwa kuhimiza makubaliano hayo ya amani yaliyosainiwa mwaka uliopita kusonga mbele baada ya ucheleweshaji wa mara kwa mara. Vita vya wenyewe vya miaka mitano, vimesababisha vifo vya karibu watu 400,000 na mamilioni kupoteza maisha yao.

Upinzani ulisema Machar hatorudi nyumbani kuunda serikali ifikapo tarehe iliyopangwa ya Novemba 12, isipokuwa kuwako na mpangilio madhubuti wa usalama.

Kabla Machar kurudi jeshi la pamoja la wanajeshi 41,500 wa upinzani na wa serikali linalazimika kutayarishwa pamoja na kikosi cha ulinzi cha pamoja cha wanajeshi 3,000 kulinda watu muhimu. **DW**

## Bobi Wine: Museveni anaongoza kwa mtutu wa bunduki

**KAMPALA,** Uganda

KIONGOZI wa upinzani nchini Uganda, Bobi Wine amemjibu Rais Yoweri Museveni ambaye katika mahojiano na Shirika la Utangazaji la BBC alimtaja kuwa adui wa maendeleo nchini humo.

Bobi Wine ambaye jina lake kamili ni Robert Kyagulani, hivi majuzi alitangaza kwamba atamkabili Rais Museveni mwenye umri wa miaka 75 katika kinyang'anyiro cha urais katika uchaguzi wa mkuu wa mwaka 2021. Rais huyo wa Uganda amekuwa madarakani tangu 1986.

Katika ujumbe wake katika mtandao wa twitter Bobi Wine alimtaja Rais Museveni huyo kuwa adui wa Uganda ambaye anaongoza kupitia mtutu wa bunduki.

Katika mahojiano hayo, Rais Museveni alidai kwamba msanii huyo wa muziki alikuwa amesema katika ziara yake Marekani kwamba watu hawafai kwenda Uganda na kuwekeza.

Katika taarifa ambayo alisema huenda rais huyo alikuwa akizungumzia mnamo Septemba 2018 katika mahojiano na Al jazeera, alisema kwamba: "Wamarekani wanafaa kuwa na wasiwasi wa kumpatia Museveni ufadhili wa kijeshi kwa kuwa ufadhili huo hautumiki kuwalinda raia wa Uganda." **BBC**

# Mwalimu mbunifu aipa shule sura mpya

**Na Yasmin Protace**

MWALIMU katika Jiji la Dar es Salaam, ameacha alama ya aina yake katika Shule ya Msingi Bongoyo baada ya kuhamasisha ukarabati ambao umebadili sura ya shule hiyo.

Hatua hiyo imewagusa walimu, wanafunzi na uongozi wa Manispaa ya Kinondoni.

Mwalimu huyo alichukua jukumu la kutafuta mfadhili ambaye amefanya ukarabati mkubwa ikiwamo kupaka rangi madarasa yote nje na ndani, kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama, ununuzi na ukarabati wa samani mbalimbali, kuanzishwa kwa maktaba ya kisasa yenye vitabu mbalimbali na vifaa vya kisasa vya kusomea, na ufundishia na ununuzi wa vifaa vya darasa la chekechea.

Akizungumza wakati wa ziara ya kushtukiza ili kujionea maajabu ya mwalimu huyo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Benjamin Sitta, ambaye ni Diwani wa Kata ya Msasani, alimpongeza mwalimu huyo kwa moyo wake wa kipekee wa kuwajali wanafunzi na walimu wenzake na kuongeza kuwa juhudi kama hizo zinastahili kutambuliwa na wadau mbalimbali kwani sio jambo la kawaida.

"Nimeguswa sana na tukio hili kwani huwa napita tu barabarani, lakini sikujua kama kuna mambo makubwa hivi yanafanyika katika shule yetu hii. Hii ni shule ya serikali, lakini imepewa sura mpya na kuifanya ifanane na shule binafsi kwa ubora. Hii itaisaidia serikali kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika katika ukarabati huu ili zitumike kwingine," alisema.

Meya huyo alitoa wito kwa wadau wengine wa maendeleo waige mfano huo na kuwekeza katika miradi ambayo itakuwa na faida kwa jamii huku akiongeza kuwa serikali ina bajeti finyu sana ya kuweza kuhudumia kila jambo hivyo wanapojitokeza wadau mbalimbali kusaidia ni jambo jema.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Aloyce Benjamin, mfadhili huyo amepaka rangi madarasa yote, amehakikisha kuna majisafi na salama, ameweka maktaba ya kisasa, amekarabati vyoo ambavyo hapo awali vilikuwa na hali mbaya sana na kuboresha darasa la shule ya awali.

"Kabla ya msaada huu, vyoo vilikuwa na hali mbaya sana hasa ukizingatia kuwa maji yalikuwa ya shida, wanafunzi wetu walikuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko lakini sasa hali ni shwari kabisa," alisema.

Alisema mabadiliko haya pia yamechochea matokeo mazuri kwani shule hiyo imefanya vizuri katika mitihani ya darasa la saba ambayo matokeo yake yameshatangazwa kwani wanafunzi wote wamefaulu kutokana na mazingira mazuri yaliyowapa motisha mkubwa.

Mwalimu aliyejitolea kuleta mabadiliko hayo kwa kutafuta mfadhili, Badru Musoke, alisema kutokana na kufanya kazi katika shule hiyo kwa muda mrefu, aliguswa na hali ya awali ambayo ilimsukuma kutafuta mfadhili na kuangalia namna ya kuboresha shule hiyo baada ya kuushirikisha uongozi wa shule.

"Nilijiunga na shule hii mwaka 2004, miaka miwili tu baada ya kuanzishwa kwake kwa hivyo naelewa vizuri changamoto zilizokuwapo na niliona ni jukumu langu kutafuta namna ya kutatua changamoto hizi ili kuyaboresha mazingira ya shule," alisema.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, kila mmoja anaweza kuleta maendeleo katika eneo lake badala ya kuisubiri serikali ifanye kila kitu.

Kabla ya mafanikio haya ya kuboresha shule, Badru aliwahi kutangazwa mwalimu bora katika Manispaa ya Kinondoni na alipokea tuzo maalumu kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.

Blandina Ibrahim na Hanno William, wanafunzi katika shule hiyo, walisema maboresho yaliyofanyika katika shule yao ni kichocheo kikubwa kwao kufanya bidii kwani mazingira ya kusoma yamekuwa bora zaidi.



Makatibu wakuu kutoka Sekta za Mazingira, Maliasili na Uvuvi kutoka kushoto, Mhandisi Joseph Malongo, Dk. Aloyce Nzuki, Prof. Adolf Mkenda na Dk. Rashid Tamatamah wakikagua maandalizi ya mkutano wa mawaziri wa SADC wa Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii jana, katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC). Makatibu wakuu hao wameridhishwa na maandalizi ya mkutano huo ambayo yamekamilika kwa asilimia 100. **PICHA NA CYNTHIA MWILOLEZI, ARUSHA**

# Aagizo watumishi watano kukamatwa

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ameiagiza kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Morogoro kuwaweka ndani na kuwahoji watumishi watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa kutuhumiwa kufanya matumizi mabaya ya fedha za Ujenzi Hospitali ya Wilaya hiyo ambao haujakamilika.

Alitoa agizo hilo baada ya kufanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya hiyo yenye lengo la kufuatilia maagizo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyoyatoa wakati wa ziara yake mkoani hapa Septemba 18, mwaka huu.

Waziri Mkuu Majaliwa alipotembelea ujenzi wa Hospitali hiyo ya Wilaya alikuta ujenzi wa hospitali hiyo haujakamilika na pia ukiwa chini ya kiwango, huku halmashauri hiyo ikiwa na maombi ya kuomba fedha za Sh. milioni 770 ili kumalizia ujenzi huo wakati maeneo mengine yenye mradi kama huo hapa nchini yakiwa yamekamilisha ujenzi kwa kiwango kilichotolewa na serikali.

Baada ya kujionea hali hiyo Waziri Mkuu aliagiza kukamilisha ujenzi huo haraka, lakini alionya kuwa Serikali Kuu haitaleta fedha yoyote kwa ajili ya kumalizia ujenzi huo badala yake aliagiza halmashauri ihusike kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo kwa kutumia fedha zake za ndani.

Maagizo hayo ndiyo yaliyompeleka Mkuu wa Mkoa kuangalia kama yametekelezwa ama la na kukuta kwa asilimia kubwa hayajatekelezwa.

Baada ya kupata taarifa hayajatekelezeka aliamua watumishi hao waliusishwa kukamatwa mara moja na kuhojiwa na kisha wale wote ambao wamebainika kuhusika kutumia fedha hizo tofauti na malengo yaliyokusudiwa na serikali warudishe ili kukamilisha ujenzi huo.

# Watanzania wahimizwa kujua haki zao

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wamehimizwa kujitokeza kwa wingi katika mikoa yote ili kuzijua haki zao za kisheria, katika kila jambo na sio kusubiri hadi kunapojitokeza matatizo yanahitaji ufumbuzi wa kisheria.

Imeelezwa kuwa matatizo yanapotokea ndipo wanahangaika kutafuta mawakili, na wengi kujikuta wanashindwa kumudu gharama za mawakili, hivyo kupoteza haki zao, bila kujua uwepo wa msaada wa kisheria.

Wito huo umetolewa leo mjini Bariadi mkoani Simiyu na msajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria, toka Wizara ya Katiba na Sheria, Felister Joseph Mushi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya mwaka huu ya Wiki ya Msaada wa Kisheria, itakayoandikishwa kitaifa wilayani hapo sambamba na maadhimisho kama hayo katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mushi amesema, wananchi wengi wa kawaida hawazijui haki zao na wengi huwa hawajishughulishi kuzijua haki zao, mpaka pale wanapopata matatizo ya kisheria, hivyo amewasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kuhudhuria maadhimisho hayo ili kupata elimu ya ufahamu wa jinsi ya kupata msaada wa kisheria, pale wanapokumbwa na matatizo ya kisheria na sio kusubiri tatizo litokee ndipo wahangaikie ufumbuzi.

Mushi alisema lengo la maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya 'Msaada wa Kisheria kwa Maendeleo Endelevu', ni kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi, ila maadhimisho ya mwaka huu hayataishia katika utoaji tu wa elimu kwa umma, ingawa yatakwenda sambamba na utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kisheria kwa watendaji wa ngazi mbalimbali na kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi, wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili wa kujitegemea.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

### KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA



115469402

**NDESHUKURWA AKYOO TUNGARAZA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria au Passport yenye namba **AB662196** iliyotolewa mwaka 2013 na Ofisi za uhamiaji Ofisi za dar es Salaam. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/394914/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



115469002

**RICHARD KHAMSINI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0609-0088** kilichotolewa na MATAI SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SUM/RB/5027/2013.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Anaitwa **YUSUFU SAIDI MTEKETA** Amepotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA MARK II Yenye usajili wa namba **T 541 AMC.** Yenye chasis namba **SX800009339** na injini namba **4S0196730.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi RB namba **MOR/MOR/RB/390548/2019.**

215469102

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 363..2014**

**Mdai:................................. ASHERI MAHERERE**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: ..........ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Kwa: ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Ombi la Mdai: ASHERI MAHERERE**

**Madai ya: PESA SHILINGI 967,500/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.


Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 06 mwaka 2019.



115469502

### KUPOTEA KWA CHETI



115467002

**Francisca John Kihengele** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **P.0741/0511** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari Itende.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/380741/2019**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LICHA YA KUFUNGWA, ZIDANE HAOGOPI



**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amekataa kusema "anahofu" baada ya Real Madrid kufungwa na Real Mallorca, lakini amewataka wachezaji wake kuendelea kuonyesha kiwango chake.

Mwanzo wa Madrid wa kutofungwa kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu ulimalizwa pale kwenye Uwanja wa Son Moix Jumamosi, shukurani kwa bao la Lago Junior.

Kikosi hicho cha Zidane kiliifunga Granada ambayo kwa sasa ipo kwenye kiwango kizuri mabao 4-2 kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini kikosi hicho kilikuwa na wakati mgumu wa kushinda kufunga dhidi ya Mallorca na kichapo hicho kimewaacha nyuma ya vinara Barcelona kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania.

Zidane kocha wa Real Madrid amesema kwamba, kutokuwa na kiwango mwendelezo ndio kumeifanya timu yake hiyo kushindwa kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tatizo ni kwamba tunaonyesha kiwango kizuri baada ya siku tatu, halafu tunashindwa kuwa na mwendelezo wake," alisema Zidane baada ya mchezo huo. "Hilo linatufanya kuwa na wakati mgumu zaidi kwetu.

"Siwezi kusema kwamba, ninahofia kwa sababu silipendi neno hilo, lakini kama tunataka kushinda kitu msimu huu, tunatakiwa kuwa na kiwango cha mwendelezo."

Madrid walikuwa bila majeruhi, Toni Kroos, Luka Modric, Gareth Bale na Lucas Vazquez, huku Luka Jovic akishindwa kuonyesha maajabu yoyote katika mchezo wake wa tatu, wakati Zidane akitumia mfumo wa 4-4-2.

Zidane alisisitiza kutokuwapo kwa wachezaji hao sio sababu ya wao kushindwa kupata matokeo mazuri kwenye mchezo huo.

# Ancelotti: Nitampigia Ibrahimovic aje Napoli

**NAPLES,** Italia

CARLO Ancelotti ametania kwamba atampigia simu Zlatan Ibrahimovic kuhusu kuhamia Napoli baada ya ushindi wa Jumamosi wa mabao 2-0 dhidi ya Hellas Verona.

Nyota huyo wa LA Galaxy, Ibrahimovic alizungumzia nafasi ya kurudi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 akionyesha nia yake ya kutaka kucheza kikosi cha Ancelotti, Napoli.

Mchezaji huyo wa zamani wa Juventus, Inter na AC Milan, amedai anaweza kufunga mabao 20 nchini Italia kwa msimu mmoja wakati wa mahojiano yake na gazeti la Gazzetta dello Sport.

Akijibu kauli hiyo ya Ibrahimovic baada ya Arkadiusz Miliak kuifungia mabao mawili Napoli dhidi ya Verona, kocha Ancelotti aliiambia Sky Sport Italia: "Nitampigia simu usiku na kumwambia tunamsubiri!

"Ni mchezaji anayenivutia zaidi, nilimwona akifunga mabao 29 kwenye mechi 30 za MLS.

"Kesho (jana), baada ya kumpigia, nitawajulisha nini kimeendelea!"





# Joao aipa pigo Atletico

**MADRID,** Hispania

JOAO Felix atakuwa nje ya dimba baada ya kuumia kifundo cha mguu kwenye mchezo dhidi ya Valencia, klabu ya Atletico Madrid imethibitisha.

Mchezaji huyo raia wa Ureno, ambaye alijiunga na Atletico kwa ada ya euro milioni 126 kutoka Benfica kipindi cha majira ya joto, aliumia kwenye mchezo wa Jumamosi wa sare ya kufungana bao 1-1 pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 alionekana kuchechemea baada ya kukwatuliwa na Dani Parejo na ilikiacha kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone kikiwa na wachezaji 10 uwanjani, baada ya kumaliza kuwatumia wachezaji wake wote watatu wa akiba.

Kocha huyo wa Atletico, Simeone alisema baada ya mchezo huo kwamba, majeruhi ya Felix "yanaweza kuwa makubwa" na vipimo vimeonyesha kwamba ameumia kifundo cha mguu.

"Joao Felix alifanyiwa vipimo vya X-ray na MRI kwenye kliniki ya Universidad de Navarra na ripoti zinaonyesha kwamba ameumia kifundo cha mguu wa kulia kwa ndani," alisema kocha huyo wa Atletico wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Bado haijajulikana atakuwa nje ya uwanja kwa muda gani, ingawa taarifa za awali zinasema kwamba, anaweza kuwa nje kwa wiki zaidi ya mbili.

Joao anaweza kuzikosa Bayer Leverkusen, Athletic Bilbao, Deportivo Alaves na Sevilla.

Tangu atue hapo kwa ada iliyoweka rekodi ya klabu, mshambuliaji huyo amefunga mabao mawili na kutoa pasi ya mwisho moja.

# Guardiola: Ratiba ya EPL ngumu

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Pep Guardiola amesema kuwa, ratiba inayokuja ya Ligi Kuu England kwa Desemba itakuwa ngumu mno kwa upande wa kikosi chake.

Guardiola amesema wachezaji wake sasa watalazimika kuwekwa kwenye friji ili kuwapoza na muda wa kucheza mechi mara kwa mara.

Kocha huyo raia wa Hispania alisema hakuna namna nyingine zaidi ya kuwaweka wachezaji wake kwenye friji ili kujipoza, kwa sababu watakuwa na mechi mbili ndani ya saa 46 katika ratiba yao hiyo ya Desemba.

Guardiola alisema kitu pekee cha kufanya baada ya mechi yao dhidi ya Wolves katika usiku wa Desemba 27 ni 'kuwaweka wachezaji kwenye friji'.

Kwa sababu baada ya hapo atakuwa na mechi dhidi ya Sheffield United katika muda usiofika siku mbili.

Guardiola alisema: "Wachezaji watakaa kwenye friji. Sitanii. Waende nyumbani, wafungue friji zao, waingia na kukaa huko kwa saa zote, kisha tuonane Etihad. Ratiba kama hii iliwahi kutokea kwenye msimu wangu wa kwanza hapa.

"Nadhani tulicheza Anfield Desemba 31 na kisha tukaenda kucheza na Burnley Januari 2. Ndiyo hivyo."

Guardiola anafahamu mtihani unaomkabili msimu huu katika kupunguza pengo la pointi baina ya timu yake ya Manchester City na Liverpool, ambapo kabla ya mechi yao ya juzi Jumamosi kuwakabili Crystal Palace ugenini pengo lilikuwa pointi nane.

"Mimi nawaonea huruma wachezaji. Hii ni biashara. Watu hawawajali wachezaji," alisema Guardiola.





# MATIP AJIFUNGA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

JOEL Matip amesaini mkataba wa muda mrefu na Liverpool utakaomwezesha kuwatumikia wababe hao wa Ligi Kuu England hadi mwaka 2024.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 28, ameshafunga mabao mawili katika michezo tisa aliyocheza msimu huu, na amekuwa kivutio kikubwa kwa kocha, Jurgen Klopp aliyemsajili mwaka 2016 akitokea Schalke 04 ya Ujerumani.

Msukumo mkubwa wa kusaini mkataba wa muda mrefu kwa beki huyo kutoka Cameroon, umetoka kwa Klopp ambaye anahitaji huduma yake kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Msimu uliopita Matip alifanya kazi kubwa katika michezo ya ligi hiyo na kusaidia mafanikio ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa kuifunga Spurs katika mchezo wa fainali.

"Nina hisia nzito za furaha moyoni mwangu, tukio la kusaini mkataba wa muda mrefu wa kuendelea kuitumikia Liverpool limenipa faraja," alisema Matip.

"Liverpool ni klabu kubwa, kila mchezaji anatamani kuwa hapa, kwangu ni bahati kuendelea kuwa sehemu ya kikosi cha mabingwa wa Ulaya, ninaahidi nitapambana zaidi ya ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita."

Matip alikosa michezo miwili iliyopita ya Ligi Kuu England, kwa sababu ya majeruhi yaliyomsibu.

# PSG yajiandaa kuizidi Real

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain inajiimarisha zaidi katika mchakato wa kumwania nyota wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen ambaye anawaniwa na Real Madrid, gazeti la Daily Mail limeandika.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, wamesema kuwa wako tayari kufanya lolote kuhakikisha kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27 anatua katika klabu yao.

Huku ikijiimarisha na mchakato huo, Madrid pia inajiandaa kuvunja mkataba wake na mshindi wa taji la Kombe la Dunia, Julian Draxler.

Madrid inatajwa pia inajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 22.5 kwa ajili ya kumsajili Leandro Paredes ili kuziba nafasi itakayoachwa na Draxler klabuni hapo.

Kiungo huyo raia wa Denmark amekuwa akichanganyikiwa baada ya hivi karibuni, Spurs kukacha ofa iliyotua klabuni hapo.

Inaelezwa kuwa mkataba wa Eriksen unatarajiwa kumalizika katika kipindi cha majira ya joto mwakani.

Jambo la kufurahisha kwa PSG ni kuwa, kwa sasa, kanuni zinamruhusu Eriksen kusaini mkataba wa awali na klabu yoyote ya nje ya England ifikapo Januari.

PSG pia wanatajwa wanamhitaji nyota wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma, gazeti la L'Equipe la Ufaransa limeripoti.

# D OO ZA SOKA
## M ZETI YA U AYA



# SOLSKJAER KUENDELEA KUPETA MAN UNITED

**Bosi wake afunguka kuwa kocha huyo amerudisha nidhamu katika kikosi cha United...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekingiwa kifua na uongozi wa klabu hiyo, kwa kupewa nafasi ya kuendelea kupanga mikakati yake ya muda mfupi na mrefu.

**Solskjaer amekuwa katika wakati mgumu wa kulinda kibarua chake kwenye siku za hivi karibuni, baada ya msukumo mkubwa uliokua ukitolewa na mashabiki wa United, kutokana na matokeo yasiyoridhisha.**

Kocha huyo raia wa Norway ameshinda michezo mitano kati ya 23 ya mwisho na kuifanya United kwa sasa kuwa alama mbili juu dhidi ya timu zilizopo kwenye shimo la kushuka daraja.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo yenye maskani yake Old Trafford imeeleza kuwa, uongozi unaelewa mipango ya meneja huyo, na hauangalii matokeo yaliyopatikana siku za karibuni.

Makamu Mwenyekiti, Ed Woodward na wamiliki wa timu, familia ya Glazers kwa asilimia 100 wanamsapoti Solskjaer na hawatafanya mabadiliko yoyote ya benchi la ufundi, hata kama jana watapoteza mechi dhidi ya Liverpool.

Woodward, ambaye kauli yake inaonekana kama kijembe kwa makocha waliopita alisema: "Ole amerudisha nidhamu kwenye timu kitu ambacho kilikosekana kwa miaka ya karibuni.

"Anajenga kikosi kitakachoheshimu historia ya klabu, huku wachezaji wakipambana na kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe. Hakuna mchezaji mkubwa kuliko klabu.

"Mipango ya Ole ndio dira yetu kwa sasa. Lazima tushinde mataji, tucheze soka la kushambulia na kuwapa vijana nafasi. Katikati ya msimu uliopita, baada ya Ole kutua, alituonyesha mahali tunapotakiwa kwenda. Tumeona timu ikicheza soka la kasi na mtiririko mzuri."

## ZISIKUPITE

### STERLING KUNEEMEKA

MANCHESTER City inajiandaa kumpa mkataba mpya ambao utamfanya mshambuliaji wake, Raheem Sterling alipwe mshahara wa pauni 450,000 kwa wiki ili kuzuia mpango wa Real Madrid kumnasa nyota huyo anayeichezea pia Timu ya Taifa ya England. ***(Star)***

### PSG, MADRID VITANI

PARIS St-Germain itachuana na Real Madrid katika mchakato wa kumsajili kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Mail on Sunday)***

### SOLSKJAER MAJARIBUNI

HATIMA ya Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, itajulikana endapo mchezaji huyo wa zamani wa timu hiyo na raia wa Norway atashindwa kufikia malengo ya Old Trafford. ***(Metro)***

### FERGUE, SOLSKJAER WATETA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, alionekana akifanya mazungumzo na Solskjaer kwenye viwanja vya mazoezi vya timu hiyo iliyokuwa inajiandaa kuikabili Liverpool hapo jana. ***(Manchester Evening News)***

### 'TUTAMUUZA KOULIBALY'

MWENYEKITI wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amekiri kuwa "itafika muda" ambao klabu hiyo italazimika kumuuza beki wake wa kati Msenegali, Kalidou Koulibaly (28), ambaye anahusishwa na mipango ya kujiunga na Manchester United. ***(Sky Sports Italia, via Sunday Express)***

### PEREZ, CEBALLOS WAKUTANA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), yuko katika mazungumzo na Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, kuhusu kutaka kuufanya uhamisho wake wa mkopo kwa Arsenal kubadilika na kuwa mkataba wa kudumu. ***(El Desmarque, via Mail on Sunday)***

### FERGUSON ANUKIA SPURS

MABOSI wa Tottenham wameweka wazi nia yao ya kumwania beki wa West Brom, Nathan Ferguson, ambaye ana umri wa miaka 19 na anatajwa kuwindwa na klabu ya Crystal Palace. ***(Sun on Sunday)***

### VILLA: MCGINN HAUZWI

KOCHA wa Aston Villa, Dean Smith, amesema kuwa klabu hiyo haina mpango wowote wa kumuuza mchezaji wa Timu ya Taifa ya Scotland, John McGinn, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sunday Express)***

### CITY, BARCA VITANI

MANCHESTER City na Barcelona zote zimetajwa kumwania kiungo wa Anderlecht, Albert Sambi Lokonga, ambaye ana umri wa miaka 19 na pia anahusishwa na mpango wa kuhamia Sevilla. ***(Marca)***

### MATIC MAMBO SAFI

MANCHESTER United inajiandaa kumpa mkataba mpya wa mwaka mmoja kiungo wa Timu ya Taifa ya Serbia, Nemanja Matic, ili kuondoa wasiwasi wa kumpoteza akiwa mchezaji huru katika kipindi cha majira ya joto mwakani. Inter Milan inatajwa kumwania mchezaji huyo. ***(Corriere dello Sport, via Sunday Express)***

## Athumani kinara wa drafti Iringa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MCHEZAJI Juma Athumani ameibuka mshindi katika fainali ya mashindano ya drafti maarufu 'Fadhili Ngajilo Draft Game Championship' yaliyofanyika kwenye Manispaa ya Iringa na kujipatia zawadi ya Sh. 500,000.

Mshindi huyo ambaye anajulikana kwa jina maarufu la 'Kulijua' kutoka katika klabu ya MR, alikabidhiwa zawadi yake juzi usiku kwenye Ukumbi wa Olefea na aliyekuwa mgeni rasmi wa mashindano hayo, Mahmoud Mgimwa, ambaye ni Mbunge wa Mufindi Kaskazini mkoani hapa.

Nafasi ya pili katika mashindano hayo ilikwenda kwa Iddy Myovelwa ambaye alizawadiwa Sh. 300,000.

Kwa upande wake, mdhamini wa mashindano hayo, Fabian Ngajilo, aliwashukuru wachezaji wote walioshiriki katika mashindano hayo ambayo yalianza kupoteza umaarufu wake.

"Drafti ni mchezo unaotumia akili nyingi sana, niiombe serikali na wadau mbalimbali wajikite kusaidia mchezo huu, ili uweze kusonga mbele, pia nawahimiza vijana wajitokeze kwa wingi kushiriki mchezo huu ambao utawasaidia kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya na bangi," alisema Ngajilo.

## Ndayiragije njia panda Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Azam FC, uko katika hatua za mwisho za kuvunja mkataba na Kocha wake, Etienne Ndayiragije (pichani chini), kwa lengo la kuweka mbele maslahi ya taifa, imefahamika.

Uamuzi wa Azam kutaka kuachana na Ndayiragije, unatokana na kuhitaji kumpa nafasi nzuri Mrundi huyo kuitumikia Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo amefanikiwa kuipeleka kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Hata hivyo, taarifa zinasema kuwa, Ndayiragije, hakuwa tayari kuacha kibarua cha kuinoa Azam FC, kwa kuwaeleza mabosi wake hao kwamba anaweza kufanya kazi zote mbili.

Chanzo chetu kinaeleza kuwa, Azam iko katika hatua za mwisho za kumtangaza aliyekuwa kocha wake, Aristico Cioba, kubeba mikoba ya Mrundi huyo ambaye alitua klabuni hapo akitokea KMC.

Kocha huyo pia alishindwa kuitumikia vizuri, Azam ambayo ilitolewa mapema katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.



# ZIMAMOTO FC WATAMBA KUENDELEZA 'DOZI' Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar, Zimamoto wamesema kuwa wataendelea kutoa "vichapo" katika kila mechi watakayocheza kwenye ligi hiyo, yenye timu 16 ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kubakia kileleni na kutetea ubingwa wanaoushikilia.

**Kauli hiyo ya Zimamoto, imekuja baada ya juzi kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 katika mechi yao ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Polisi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan.**

Zimamoto inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 16 sawa na KMKM, lakini wao wakiwa na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Hassan Abdulrahman, alisema kuwa walifanya maandalizi mazuri kabla ya kuanza kwa msimu huu, kwa sababu walitaka kuwa na matokeo chanya katika kila mechi watakayocheza.

Abdulrahman alisema kuwa timu yao imeanza vizuri msimu huu, ikiwa mpaka sasa haijapoteza mchezo, ikiwa imeshinda michezo mitano na kutoka sare mchezo mmoja uliochezwa Kisiwani Pemba dhidi ya Selem View.

"Tumejiandaa vya kutosha kuhakikisha tunabakia kileleni, bado ninaamini timu yangu itaendelea kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, tuna kikosi imara, tulijipanga kwa sababu tunajua ligi itakuwa ngumu," alisema Abdulrahman.

Kiongozi huyo alisema kuwa ushindani katika ligi hiyo umeongezeka, lakini wamewaandaa wachezaji wao kucheza kwa tahadhari kwa sababu wanahitaji kuchukua taji la ligi hiyo kwa mara nyingine tena.

"Japo ni mapema mno kusema kama tunataka ubingwa au hapana, lakini ni mapema kusema kama hatutofungwa, ili sisi malengo yetu makubwa ni kuhakikisha timu inaendelea kufanya vizuri kama tulivyoanza, maana timu za Zanzibar, hasa zinazoshiriki Ligi Kuu huwa hazitabiriki," alisema kiongozi huyo.

Ligi hiyo ndiyo hutoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo hufanyika kila mwaka.



Beki wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Erasto Nyoni, akielekea kwenye basi la timu hiyo muda mfupi baada ya kikosi cha Stars kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi wakitokea Sudan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Bandari D'Salaam waibuka kidedea*

**Na Ashton Balaigwa,** Morogoro

TIMU ya Bandari Dar es Salaam imefanikiwa kutwaa ushindi wa jumla katika mashindano ya 13 ya Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Mashindano hayo yalifanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri wa Morogoro mkoani hapa, na mgeni rasmi alikuwa ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mohammed Ahmada Salum, ambaye aliwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari la Zanzibar, Abdallah Juma Abdallah.

Kabla ya kukaribishwa kwa mgeni rasmi kufunga mashindano hayo, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa TPA, Gabriel Mwita, alisema kuwa jumla ya wanamichezo 503 walishiriki mashindano hayo ambayo yameshirikisha timu za Bandari Makao Makuu, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Maziwa ( Victoria, Tanganyika na Nyasa), Zanzibar na wengine kutoka Ticks.

Mwita alisema kuwa wanamichezo hao walichuana katika michezo mbalimbali ikiwamo soka, netiboli, riadha, mbio za kupokezana vijiti, kurusha tufe, kurusha mkuki, kuvuta kamba pamoja na bao.

"Mamlaka ya Bandari inafanya michezo hii kuwa endelevu kwa ajili ya kutoa fursa kwa wafanyakazi kushiriki katika michezo, ikiwa ni kutekeleza sera ya serikali kutokomeza magonjwa yasiyo ya lazima kwa kufanya mazoezi," alisema Mwita.

Timu ya Netiboli ya Bandari Zanzibar iliibuka mabingwa katika mchezo huo kwa kutopoteza mechi hata moja baada ya kuwafunga wenzao kutoka Mtwara, Tanga, Bandari za Maziwa, Makao Makuu na Bandari Dar es Salaam.

Kwa upande wa soka, Bandari Dar es Salaam ilitwaa ubingwa wa mwaka huu baada ya kuifunga Bandari Zanzibar kwa mabao 2-0, huku bingwa mtetezi Bandari ya Maziwa ikivuliwa taji hilo katika hatua za awali za mashindano hayo.

Michezo
Jumatatu Oktoba 21, 2019
Nipashe



Matip ajifunga Liverpool

UKURASA 29



Beki wa Chelsea, Fikayo Tomori (kulia), akijiandaa kumtoka beki mwenzake wa Newcastle United Mholanzi Jetro Willems katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Stamford Bridge jijini London juzi, Jumamosi. Chelsea ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# VAR kutumika Simba vs Yanga

## TFF yapanga kumaliza utata wa waamuzi katika mechi hiyo, yateta na Wachina kuja...

**Na Isaac Kijoti**

KWA mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania kama si Afrika Mashariki kwa ujumla, Watanzania wanaweza kushuhudia Teknolojia ya Video ya Kumsaidia Refa (VAR) ikitumika nchini kwenye mechi ya Simba na Yanga.

**Ili kuondoa lawama na shutuma kwa mwamuzi ambazo zimekuwa zikijitokeza katika mechi ya watani hao wa jadi, Shirikisho la Soka nchini (TFF), lipo katika mchakato wa kuhakikisha VAR inatumika katika mechi mbili Simba na Yanga zitakapokutana.**

Akizungumza katika mkutano wa wahariri wa michezo wa vyombo mbalimbali vya habari nchini uliofanyika jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema wapo katika mazungumzo na wataalamu wa teknolojia hiyo kutoka barani Asia.

Kidao alisema tayari wamezigusia klabu husika, Simba na Yanga kuhusu mpango huo na kwamba pamejitokeza mvutano kidogo ila wanaendelea kujadiliana.

"Tulipokuwa katika mkutano wa Caf (Shirikisho la Soka Afrika) tulikutana na wahusika tukazungumza nao na kututajia gharama kwa mechi moja ni Dola za Marekani 4,500 (zaidi ya Sh. milioni 10 za Tanzania). "Ni gharama ambazo tunaweza kuzimudu ili kuleta ufanisi na zaidi kuondoa lawama na shutuma zilizozoeleka kwa waamuzi zinapokutana timu hizo," alisema Kidao.

Alisema pamoja na kutaka kushughulikia mchakato huo viongozi wa klabu hizo wamegawanyika huku baadhi wakionekana kuukubali na wengine wakipinga.

"Pamoja na nia yetu nzuri bado kuna baadhi ya viongozi wa klabu hizo hawataki VAR itumike ila kwa sababu muda bado upo tunaweza kukubaliana," alisema.

Mechi ya raundi ya kwanza itakayoikutanisha miamba hiyo Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam inatarajiwa kuchezwa mapema Januari mwakani.

Katika mkutano huo ambao TFF ilikuwa ikieleza mafanikio yake ya miaka miwili chini ya Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia, mbali ya wahariri wa michezo, pia ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wa soka.

Aidha, Karia mbali ya kueleza mafanikio mbalimbali waliyoyapata ikiwa ni pamoja Taifa Stars kufuzu na kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) nchini Misri na zile za Wachezaji wa Ndani (CHAN) mwakani nchini Cameroon, alisema wamepata wawekezaji mbalimbali waliomba kujenga akademi za soka hapa nchini.

"Kuna wawekezaji kutoka yalipo makao makuu ya soka duniani, Uswisi na wengine kutoka Misri wameomba wapewe eneo la kujenga akademi za soka nchini.

"Hawa wa Uswisi tayari wameonyeshwa eneo Dodoma na hawa wa Misri tunawatafutia hapa Dar es Salaam," alisema Karia.

# Nchimbi: Nilijua nitaifunga Sudan

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na klabu ya Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi, amesema kuwa alijiandaa kufunga goli katika mechi dhidi ya Sudan, lakini furaha yake imeongezeka zaidi baada ya kufunga bao muhimu katika mchezo huo.

Nchimbi ambaye aliitwa kuchukua nafasi ya nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, aliyekuwa na udhuru kuelekea mechi ya kirafiki dhidi ya Rwanda, alifunga bao la ushindi ambalo limeipeleka Tanzania kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Akizungumza na gazeti hili, Nchimbi, alisema kuwa lengo lake la kupambana kuhakikisha anafunga, lilikuwa ni kudhihirisha uwezo wake na kutomwangusha Kocha Etienne Ndayiragije ambaye alimwamini na kumpa nafasi hiyo kwa mara ya kwanza kwenye kikosi hicho.

Nchimbi alisema pia mbali na kujipanga kuivusha Stars, aliamini mechi hiyo dhidi ya Sudan ni mwanzo wa kusaka timu nje ya Tanzania.

"Nilijua nitafunga, nilikuwa na ndoto hizo, tangu jina langu lilipojumuishwa katika kikosi cha Stars, nikawa ninajipanga kuhakikisha ninafanya kile ninachokiwaza, lakini kikubwa nilijuwa itakuwa ni bao la kuanzisha safari yangu ya kucheza soka Ulaya," alisema Nchimbi.

Aliongeza kuwa atahakikisha analinda kiwango chake, ili itakapofika fainali hizo za CHAN hapo mwakani, awe ni mmoja wa wachezaji watakaokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

"Nimeshaingia kwenye rekodi, ninajua kila mmoja atakuwa ananifuatilia, nitajituma kuhakikisha ninaendelea kufanya vema katika kila mchezo, nitakapopata nafasi, naamini wachezaji wenye vipaji ni wengi, lakini nafasi huwa chache," Nchimbi alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002